SUPA JACKPOT
TZS. 1,029,401,974
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**WAZIRI** aagiza vigogo Ardhi kuondolewa


USAWA KIJINSIA
Wanaharakati usawa kijinsia wawaambia wanahabari bebeni bango tufike 50/50
Ukurasa 12
Ukurasa 13
siasa
JUMATANO SEPTEMBA 7, 2022
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
AKIWAHAKIKISHIA AMANI NA HESHIMA ... Mteule Ruto kwenye salamu zenye vichekesho, vijembe kwa rafiki Kenyatta, mshindani Odinga
Ukimya uchaguzi viongozi CCM unavyoakisi zama mpya kisiasa
Na Ani Jozeni
UCHAGUZI ndani ya CCM miaka iliyopita ulikuwa wenye ushawishi mkubwa na kampeni za wazi, lakini mwaka huu shughuli hiyo inaendelea bila dalili za wazi kuwa chama tawala kiko katika mchakato wa kuchagua safu zake za uongozi.
Hali hiyo inaendana na kupungua kwa ushawishi wa makundi ya watia nia na wasaidizi wao au wapambe wao kutokana na kupungua siyo tu kwa mahitaji ya wananchi kwa watia nia kama hao kuleta majibu kwa masuala yanayowasumbua.
Ni hata pia kushuka uwezo wao kuinua hisia hizo kwa kutoa motisha wafanye kampeni. Huenda ni mwendelezo wa taratibu za uchaguzi za awamu ya tano.
mitaani, la hasha. Kuna mchongo wa kisiasa wa kupanuliwa uhuru.
Ndiyo maana uchaguzi wa sasa ndani ya CCM unakuwa na sura tofauti, lakini suala tangulizi siyo haya mabadiliko ya kutaka uwazi na ukweli zaidi, au uhuru mpana zaidi katika vyombo vya habari, kwani hadi sasa bado hizo ni nia chanya zinazoelezewa na Mwenyekiti wa CCM.
Bado hakuna uhakika kuwa, nje ya uwazi zaidi kiasi fulani katika utoaji na usambazaji wa habari, hali itakuwaje katika siasa, kwani upo mtindo mpya wa kuendesha siasa ambao ulishazoeleka, uliosahihisha bashasha na nderemo za nyakati zilizopita.
Suala hapa ni jinsi ya kujaza pengo hilo la uchangamfu, au labda ni vyema hali ibaki hivyo ili vyo ili wasizuke watu wakawa juu ya chama, majina yao yasipopita kuwe na hali ya hatari.
Na pia ilifikia mahali hata chama chenyewe kinashindwa kuwa na uwezo wa kusimamia ipasavyo mtiririko wa kutiania (kuchukua fomu kuchaguliwa) halafu suala

UKURASA 11

Nipashe
Jumatano Septemba 7, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581061
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kilio upigaji wa tozo maegesho

**WANANCHI** walalamika kupewa taarifa feki, wahusika wakiri... *Endelea ukurasa 2*





UKURASA WA 7


## KINANA ATAKA VIONGOZI VING'ANG'ANIZI WATOSWE

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimewataka wanachama wake kuwapiga chini viongozi ving'ang'anizi wanaotaka kubaki madarakani kwa kutumia rushwa...

UKURASA WA 8

## MAUAJI YATIKISA KILA PEMBE

NI mauaji yanayoendelea kutikisa kila kukicha kwa watu kuuana na wengine kujiua. Ripoti kutoka mikoa mbalimbali nchini kuhusu matukio yaliyotokea jana na juzi zinaeleza kuwa huko...



## Ahueni bei ya petroli yashuka



UKURASA 3

## Adha abiria usafiri, ulanguzi nauli stendi kuu ya Magufuli

UKURASA 2



Msongamano wa abiria wakisubiri usafiri katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, Mbezi Louis, mkoani Dar es Salaam jana. Tangu Ijumaa iliyopita kumekuwa na tatizo la usafiri wa kwenda mikoa ya Dodoma, Morogoro na Kanda ya Kaskazini, ambapo abiria wengi walioambatana na watoto wanaorudi shuleni walikwama kituoni hapo. **PICHA: SALOME KITOMARI**

**MICHEZO** **ZORAN ATOA NENO KUONDOKA SIMBA** UK.24 **KABWELA** UK. 18



Picha mbalimbali zikionyesha madhara ya mafuriko yaliyosababishwa na mvua ya muda mfupi katika Mtaa wa Mwembeni, Kata ya Igoma, jijini Mwanza juzi, ambapo baadhi ya wakazi wa eneo hilo, walidai kuwa hali hiyo ilitokana na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), kujenga mitaro inayoelekeza maji kwenye makazi yao. **Habari Uk. 10. PICHA: VITUS AUDAX**

# Kilio upigaji wa tozo maegesho

**Na Jenifer Gilla**

BAADHI ya wamiliki wa magari mkoani Dar es Salaam, wamelalamikia kulipishwa tozo za maegesho ya magari katika maeneo ambayo hawajawahi kuegesha kwa kipindi husika, jambo linalowapatia usumbufu.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wamiliki wa magari wameziomba mamlaka husika kuingilia kati vitendo hivyo vinavyoonekana kuota mizizi kila kukicha na kuwa kero kwao.

Damian Robert, mkazi wa Ubungo, alisema alisikia malalamiko kwa watu tofauti alipokwenda kuangalia akakuta na yeya ana deni la Sh. 10,000 la maegesho katika maeneo tofauti ambayo hajawahi kutembelea kwa muda mrefu.

"Kuna mtu alilalamikia suala hilo katika kundi la WhatsApp, nikasema ngoja na mimi niangalie, nikakuta mlolongo wa madeni 20 ya Sh. 500 ndani ya mwezi mmoja, ambayo sijawahi kufika. Mimi naishi Ubungo, nafanya kazi Mwenge na madeni yanaonyesha nimeegesha gari Kigamboni, Temeke na Posta, " alisema.

Victoria Norman, mkazi wa Kigamboni, alisema amejikuta na deni la Sh. 2,000 kwa kipindi ambacho gari lake halikutoka kwa sababu alikuwa safarini kwa muda wa wiki mbili.

"Kuna siku nilienda Kariakoo nikaegesha lakini cha ajabu sijaletewa maegesho ya hapo, nikaletewa malipo ya maegesho ya Jamhuri, Daf Fee Market na nyingine mbili za mwaka jana halafu maeneo ambayo sijawahi kwenda," alisema.

Norman alisema kinachomshangaza tozo hizo zote ni za malipo ya Sh.500 kwa maana kuwa alikaa katika hayo maeneo kwa saa moja tu jambo linaloonyesha tozo hiyo ni ya kutungwa.

Naye Sostenes Tambua, mkazi wa Kibada, Kigamboni, alisema alishangaa kutumiwa ujumbe kutoka Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA), ukimtaka alipie tozo ya maegesho wakati siku hiyo hakutoka nyumbani kabisa.

"Ni jana niliona 'reminder' (kukumbushwa) kulipia tozo ya maegesho. Nilipoiangalia nikaona inaonyesha nimeegesha gari saa 6:00 mchana maeneo ya Uhamiaji, Kurasini. Nilishtuka kwa sababu hiyo jana sijatoka nyumbani. Hii 'parking' ya saa sita inatoka wapi? Naona kama kuna mchezo hapa," alisema.

**MANISPAA ZANENA**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, Beatrice Dominic, alisema japo hajakabidhiwa mfumo huo na TARURA, atafuatilia na kufanyia kazi jambo hilo ili kuondoa kero hiyo.

"Niko njiani narudi kutoka Dodoma. Nikifika nitaweka kikao na kampuni inayohusika na maegesho ili tuone ni namna gani tunaweza kuondoa hii kero kwa sababu nilishamwita wiki iliyopita nikamwambia nasikia kuna haya malalamiko akakataa," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa wa Kinondoni, Hanifa Hamza, alisema hajawahi kufikiwa na kero ya aina hiyo lakini atatuma timu yake kufuatilia na kuitatua.

"Sasa hivi nimeunda kikosi maalum kwa ajili ya kufuatilia kero mbalimbali za wananchi ikiwamo ya aina hiyo. Kwa hiyo kama una ushahidi naomba nitumie, kisha tutakaa na watu wangu wa teknolojia ya mtandao tuone namna ya kuishughulikia," alisema.

**MAMLAKA YAKIRI**

Msimamizi wa Mradi, Web Cooperation, unashughulika na maegesho katika wilaya za Kinondoni na Ubungo, Nawak Hassan, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo linalosababishwa na watoa huduma wao kutokuwa makini wakati wa kupiga picha magari hayo.

"Tunapokea sana hayo malalamiko. Niseme tatizo lipo kwa hawa watoa huduma, hawa vijana wetu kwa sababu zao binafsi. Badala ya kupiga picha gari anapiga picha chini, halafu anaingiza namba ya gari lolote kwa hiyo unakuta hiyo bili inakwenda kwa mtu asiyehusika," alisema Nawak.

Alisema wakipokea malalamiko huwa wanaingia kwenye mfumo na kuifuta bili pamoja na kumwambia mhudumu aliyefanya kosa hilo kulipa deni hilo.

Alisema pia wako katika mchakato wa kuboresha mfumo wa kurekodi magari hayo ili uwe na uwezo wa kukataa iwapo picha ya gari haitoendana na namba za gari husika ili kuondoa hiyo changamoto.

"Niwaombe kama kuna mtu anapitia hiyo changamoto aje kwenye ofisi zetu Kinondoni na Posta tutamsaidia. Hata kama mfumo unakuonyesha kuwa ulipaki Temeka lakini Kinondoni ndiyo karibu, njoo tutawasiliana na wahusika wa huko na tutakusaidia," alisema.

# Adha usafiri, nauli juu Kituo cha Magufuli

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya shule za msingi na sekondari nchini kufunguliwa, baadhi ya wazazi wanaowapeleka watoto wao shuleni wamekumbana na kadhia ya kupanda kwa nauli katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli kilichoko Mbezi Luis mkoani Dar es Saalam.

Hali hiyo ilisababishwa na uhaba wa mabasi yaendayo mikoani, kusababisha idadi kubwa ya abiria wakikosa usafiri.

Juzi, Nipashe lilifika katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli na kuwakuta baadhi ya abiria wakiwa wanasubiri usafiri, huku wengine wakiwa wamekaa muda mrefu pasipo kujua hatima yao.

Mmoja wa abiria katika stendi hiyo, Jackson Chande, aliyekuwa akisafiri kwenda mkoani Dodoma alisema: "Nimefika kituoni saa 2:00 asubuhi nimekosa gari. Nimekaa mpaka saa 5:00 asubuhi nikaambiwa kuwa nitatafutiwa gari lingine kwa maana magari yaliyokuwapo yameshajaa."

"Leo (juzi) imekua tofauti sana mpaka mda huu sijapata gari, watu wanaosafiri ni wengi shule zimefunguliwa wengine wanaongeza hadi nauli. Hii yote ni kutokana na wasafiri kuwa wengi mpaka sasa sijajua kama nitasafiri," aliongeza.

Chande, alisema amekuwa akisafiri kwenda mkoani mara kwa mara kwa kutumia stendi hiyo, lakini kwa hali ambayo aliikuta jana haikuwa ya kawaida.

Alisema nauli ya kwenda Dodoma ni Sh. 22,000 lakini baadhi ya magari yamekuwa yakitoza hadi Sh. 35,000.

Abiria mwingine, Musa Charles, aliyekuwa anasafiri kwenda Morogoro aliieleza Nipashe kwamba alifika katika stendi hiyo saa mbili asubuhi, lakini hadi saa saba mchana hakuwa amepata usafiri.

Charles, aliongeza kwamba usafiri wa siku ya jana ulikuwa mgumu, kubahatisha kwamba mawakala wamekuwa wakifanya ulanguzi wa tiketi kwa abiria.

Alisema nauli ya Morogoro baadhi ya magari yamekuwa yakitoza kati ya Sh. 12,000 hadi 15,000.

**KAULI YA POLISI**

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilboard Mtafungwa, akizungumza na madereva wa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani juzi, aliwataka kufuata sheria za usalama barabarani hasa kipindi hiki cha ongezeko la abiria waendao mikoani ili kuepusha ajali.

Naye Meneja wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, Isihaka Waziri, akitoa ufafanuzi wa tatizo la abiria na kuchelewa kutoka kwa mabasi asubuhi, alisema Kamanda Mtafungwa alifika kituoni hapo na kutoa elimu kwa madereva, hali iliyosababisha abiria wengi kujaa kituoni.

Alisema, ongezeko la abiria limesababishwa na kufunguliwa kwa shule na kusababisha abiria kuwa wengi ndani ya stendi.

**Imeandaliwa na Owen Bariki, Victoria Mgodomi, Salma Twaha, Golden Kisapile (TUDARCo) na Evence Evarist (DSJ).**

HABARI KITAIFA

# Ahueni bei mafuta watumiaji petroli

**Na Mwandishi Wetu**

Watumiaji wa mafuta ya petroli wamepata unafuu baada ya bei mpya za ukomo Septemba, 2022 zilizotangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kupungua kati ya Sh. 271 na Sh. 362 kwa lita kulinganisha na ilivyokuwa mwezi uliopita.

Taarifa ya bei mpya iliyotangazwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Modestus Lumato, inaonyesha kwamba kupungua kwa bei hiyo kumetokana na ruzuku ya Sh. Bilioni 65 iliyotolewa na serikali.

Pamoja na kushuka kwa petroli kwa bei hizi zitakazoanza kutumika leo, dizeli imepanda kwa kati ya Sh 31 na 86 kwa lita. Pia bei ya mafuta ya taa imepungua kwa Sh. 430 kwa ujazo huo.

"Bei za mafuta katika soko la dunia za Julai, 2022 zimepungua ikilinganishwa na bei hizo kwa Juni 2022. Hivyo, bei za mafuta katika soko la ndani zimepungua vilevile kwa kati ya Sh. 271 na Sh. 362 kwa lita kwa petroli na kwa shilingi 430 kwa lita kwa mafuta ya taa kulinganisha na bei zenye ruzuku za Agosti 2022.

"Kwa mafuta ya dizeli, ukiiacha bei ya Tanga ambayo inashuka kwa Sh. 13 kwa lita, bei za Septemba 2022 zimeongezeka kwa Sh. 37 na Sh. 86 kwa lita kwa Dar es Salaam na Mtwara, sawia, ukilinganisha na bei zenye ruzuku za Agosti 2022," ilisema taarifa hiyo ya EWURA.

Kutokana na mabadiliko hayo, bei mpya kwa petroli Dar es Salaam itakuwa Sh. 2,969, dizeli Sh. 3,125 na mafuta ya taa Sh. 3,335 kwa lita wakati Tanga bei mpya kwa Tanga itakuwa Sh. 3,033 petroli na Sh. 3,131 dizeli.

Kwa upande wa Mtwara ambako shehena ya mafuta hushushwa kama ilivyo kwa Dar es Salaam na Tanga, bei mpya rejareja ya petroli itakuwa Sh. 3,082 wakati dizeli itauzwa kwa Sh. 3,213 kwa lita.



Bei mpya katika miji mingine baada ya ruzuku ni Arusha petroli Sh. 3,090 na dizeli Sh. 3,188 wakati Kibaha petroli ni Sh. 2,973 na dizeli Sh. 3,130. Bukoba ni Sh. 3,184 kwa petroli na Sh. 3,341 dizeli kwa lita.

Kigoma mjini lita ya petroli itauzwa kwa Sh. 3,131 na dizeli Sh. 3,288 huku Babati bei mpya ikiwa Sh. 3,124 kwa petroli na Sh. 3,222 dizeli. Dodoma bei mpya ni Sh. 3,027 petroli na Sh. 3,184 dizeli.

Katika mji wa Geita, bei mpya ya petroli kwa lita ni Sh. 3,134 na dizeli Sh. 3,291 wakati Iringa itakuwa Sh. 3,089 petroli na Sh. 3,195 kwa lita ya dizeli.

**•Bei mpya kwa miji yote nchini tazama ukurasa wa 4 na wa 5.**



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Prof. Mark Mwandosya (kushoto), akimsikiliza Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Cyprian Luhemeja (kulia), alipotembelea ofisi hizo, jana. Wa pili kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya DAWASA, Jenerali mstaafu Davis Mwamunyange. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri aagiza vigogo Ardhi kuondolewa

**Romana Mallya**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, ameagiza Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Rukwa, Swagile Juma, asimame kazi na atafutiwe majukumu mengine sambamba na Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Venance Mworo.

Pia, ameagiza Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Simiyu, ajitathmini na Msajili Msaidizi wa Hati Mkoa wa Mbeya atafutiwe kituo kingine kwa sababu kuna mambo yanakwenda ndivyo sivyo.

Dk. Mabula alitoa maagizo hayo jana jijini Dar es Salaam,wakati akifungua kikao kazi cha makamishna wasaidizi wa ardhi wa mikoa 26. Alisema haridhishwi na utendaji wa mkurugenzi wa TEHAMA ambaye yuko wizarani kwake.

"Tulikuwa tumekwenda kwa kasi kubwa kidogo na mpaka tunapoanzisha mfumo pale Dodoma, ni watendaji wetu wa ndani ambao wamefanya kazi ile, tofauti na ya mwanzo tuliyokasimu watu wa nje kuifanya," alisema.

Mabula, alimwagiza Katibu Mkuu awasiliane na utumishi ili wapate mtu mwingine atakayekwenda na kasi kwa sababu wasipoweka mifumo vizuri katika suala la utendaji hawataweza kumaliza migogoro.

Katika mkutano huo, Waziri alitaja mambo sita yanayoathiri utendaji kazi na kueleza kuwa wataelekeza nguvu kushughulika nayo na mengine, watachukua hatua za haraka ili kufanikisha dhamira ya wizara ya kuwahudumia wananchi kwa ufanisi.

Alitaja jambo la kwanza kuwa ni upungufu kwenye kufanya kazi kwa pamoja na kwa ushirikiano na kueleza kuwa, tatizo hilo bado liko kwenye ngazi ya mikoa na halmashauri ambapo kila mtu anafanya lake.

Jambo la pili, alisema ni maagizo au utekelezaji wa maelekezo anayotoa na kutolea mfano wa agizo lake la uhakiki wa mashamba na taarifa alitaka aipate Julai, 2022 na kwamba licha ya Katibu Mkuu kuongeza muda hadi Agosti 15, mwaka huu, ni mikoa 17 tu iliyowasilisha.

"Mikoa ambayo haijawasilisha ni Arusha, Dodoma, Geita, Kagera, Njombe, Shinyanga, Simiyu na Songwe," aliitaja.

Jambo la tatu, Waziri alisema ni watu hao kutotambua majukumu waliyopewa na baadhi yao wana upungufu wa kuelewa nini wanapaswa kufanya, wanakosa weledi na ubunifu.

"Pamoja na hatua za kinidhamu ambazo tayari zimechukuliwa kwa watumishi ikiwa ni pamoja na kuwaachisha kazi kwa mikoa ya Mbeya (watatu), na Dodoma (watatu), ninaagiza hatua zichukuliwe kwa mikoa mingine," alisema.

Pia, alisema mikoa ambayo wanakamilisha taratibu za kinidhamu kwa watumishi, siku za hivi karibuni ni Mbeya, Dar es Saaam, Mwanza na Arusha na Lindi.

Jambo la nne, alilitaja ni ushirikiano na viongozi wa mikoa na halmashauri ambapo alisema mrejesho ni mzuri lakini baadhi yao anazo taarifa za kutoshirikiana kikamilifu na viongozi wa mikoa na kuwataka wabadilike.

Mabula, alitaja jambo la tano ni weledi na uadilifu na kueleza kuwa ameanza kupokea taarifa za baadhi yao kushiriki au kwa wasaidizi wao, kukiuka maadili ya utumishi wa umma.

"Jambo la sita, ni mipangomiji na uendelezaji miji. Tumekuwa na programu ya urasimishaji makazi ya miaka 10 ambayo ilianza kutekelezwa mwaka 2013 na itakamilika mwaka 2023.

"Hatuwezi kuendelea hivyo bila kuchukua hatua. Hili naagiza likasimamiwe ipasavyo na kwa nguvu zote. Majengo yanayojengwa kinyume cha utaratibu hasa kwenye mipango miji, yasimamishwe mara moja na taratibu za hatua kwa waliotoa kibali kinyume cha utaratibu, Katibu Mkuu ninataka hatua zichukuliwe mara moja," alisema.

Waziri Mabula, alisema kumezuka vituo vya mafuta kila kona wakati kanuni zipo na zinaelekeza ni baada ya mita ngapi kijengwe kingine na kuwataka wakabadilishe kanuni kwa mijini badala ya mita 200 angalau iwe 500.

Aliagiza viwanja ambavyo vimetelekezwa vikafanyiwe kazi hadi Septemba 25, mwaka huu, apewe taarifa kutoka mikoa yote.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
06.09.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kutaarifu umma kuwa siku ya **Jumamosi tarehe 10-09-2022 hadi 14-09-2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea JNHPP SITE**, gari hizo zenye namba za usajili: **T 959 DTN / T 321 DDH T 957 DTN / T 310 DDH T 967 DTN / T 390 DHQ T 402 DFE / T 777 AQR T 645 DFA / T 416 AYQ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 23** |
| **Upana** | - | **mita 7.40** |
| **Kimo** | - | **mita 4.60** |

2. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM hadi JNHPP SITE kupitia KILWA ROAD, KIBITI, MLOKA.**
Gari litasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 06:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** **Kutoka Dar es Salaam Port mpaka Bungu.**
Kutoka **Bungu kwenda JNHPP Site** gari litasafiri muda wa mchana ***( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

217033501



**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)**

**TANGAZO LA KUAHIRISHWA MNADA WA HADHARA WA MAGARI CHAKAVU**

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kushirikiana na Ofisi ya Msimamizi Mkuu wa Mali za Serikali Mkoa wa Dar es Salaam, unawatangazia Umma kuwa mnada wa hadhara wa Magari Chakavu yaliyoko Ofisi za TASAF - Dare es Salaam uliokuwa ufanyike siku ya Jumatano tarehe 7/09/2022 umeahirisha kwa sababu zilizo nje ya uwezo wetu mpaka hapo itakapotangazwa tena.

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) unaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – TASAF**
**Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete**
**S. L. P. 2719 Dodoma, Tanzania**
**Simu: 255 026 2963866**
**Nukushi: 255 026 2963871**
**Barua pepe: info@tasaf.go.tz**
**Tofuti: www.tasaf.go.tzg**

217031602

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura — Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji — ISO 9001:2015 Certified

# KUMB: PPR/2022 - 09/1

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 7 SEPTEMBA 2022

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia Jumatano, Tarehe 7 Septemba 2022.

Bei za Mafuta katika soko la dunia za Julai 2022 zimepungua ikilinganishwa na bei hizo kwa Juni 2022. Hivyo, bei za mafuta katika soko la ndani zimepungua vilevile kwa kati ya shilingi 271/lita na shilingi 362/lita kwa petroli na kwa shilingi 430/lita kwa mafuta ya taa ukilinganisha na bei zenye ruzuku za Agosti 2022. Kwa mafuta ya dizeli, ukiiacha bei ya Tanga ambayo inashuka kwa shilingi 13/lita, bei za Septemba 2022 zimeongezeka kwa shilingi 37/lita na shilingi 86/lita kwa Dar es Salaam na Mtwara, sawia, ukilinganisha na bei zenye ruzuku za Agosti 2022. Ili kuendelea kupunguza madhara ya ongezeko la bei za dizeli hapa nchini ambapo shughuli nyingi za kiuchumi zinategemea dizeli na pia ili kupunguza tofauti kati ya bei za petroli na dizeli, Serikali imetoa ruzuku ya shilingi bilioni 65 ili kupunguza bei za mafuta za mwezi Septemba 2022. Kwa kutoa ruzuku hiyo, Serikali imepunguza bei za bidhaa za mafuta kwa mwezi Septemba 2022 kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na.1 Bei za Mafuta kwa mwezi Septemba 2022 kabla na baada ya ruzuku shilingi/lita**

| Bandari | Septemba 2022 Bei kabla ya Ruzuku | | | Septemba 2022 Bei baada ya Ruzuku | | | Kiwango cha Ruzuku | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
| Dar es Salaam | 3,049 | 3,359 | 3,335 | 2,969 | 3,125 | 3,335 | 80 | 234 | 0 |
| Tanga | 3,073 | 3,336 | - | 3,033 | 3,131 | | 40 | 205 | - |
| Mtwara | 3,122 | 3,433 | - | 3,082 | 3,213 | | 40 | 220 | - |

Kutokana na mgao wa ruzuku hiyo bei za Mafuta kuanzia tarehe 7 Septemba 2022 ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.2**.

**Jedwali Na. 2 Bei za Mafuta za rejareja kuanzia tarehe 7 Septemba 2022 – Shilingi/Lita**

| Port | Bei za Mafuta za Septemba 2022 zenye Ruzuku | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa* |
| Dar es Salaam | 2,969 | 3,125 | 3,335 |
| Tanga | 3,033 | 3,131 | |
| Mtwara | 3,082 | 3,213 | |

***Bei ya mafuta ya taa haina ruzuku**

Katika kutekeleza bei hizi, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta watatakiwa kuzingatia yafuatayo: -

(a) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba *152*00# na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(b) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166,** bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(c) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (Price cap) au kushuka chini ya **bei iliyoruhusiwa *(Floor Price)* kama ilivyokokotolewa kwa kutumia fomula na Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa kupitia Magazeti ya Serikali Na. 2A na 57 ya tarehe 3 Januari 2022 na 28 Januari 2022, sawia.**

(d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(e) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (Electronic Fiscal Pump Printers) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

**(f) Wauzaji wa Mafuta ya petroli wa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei yenye ruzuku kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 3. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili**

**(g) Wauzaji wa bidhaa za mafuta kwa jumla wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei yenye ruzuku kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 4. Isipokuwa kwa wateja ambao wana msamaha wa kodi. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.**

**JEDWALI 3: BEI KIKOMO ZA REJAREJA (SHS./LITA)**

| Mji | Bei ya Petroli isiyo na Ruzuku | Bei ya Petroli yenye Ruzuku | Bei ya Dizeli isiyo na Ruzuku | Bei ya Dizeli yenye Ruzuku | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|---|---|
| **Dar es Salaam** | **3,049** | **2,969** | **3,359** | **3,125** | **3,335** |
| **Arusha** | **3,130** | **3,090** | **3,393** | **3,188** | **3,419** |
| Arumeru (Usa River) | 3,130 | 3,090 | 3,393 | 3,188 | 3,419 |
| Karatu | 3,148 | 3,108 | 3,411 | 3,206 | 3,438 |
| Longido | 3,141 | 3,101 | 3,404 | 3,199 | 3,430 |
| Monduli | 3,135 | 3,095 | 3,398 | 3,193 | 3,425 |
| Monduli-Makuyuni | 3,140 | 3,100 | 3,403 | 3,198 | 3,430 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 3,214 | 3,174 | 3,477 | 3,272 | 3,511 |
| **Coast (Kibaha)** | **3,053** | **2,973** | **3,364** | **3,130** | **3,340** |
| Bagamoyo | 3,060 | 2,980 | 3,370 | 3,136 | 3,346 |
| Bagamoyo (Miono) | 3,090 | 3,010 | 3,401 | 3,167 | 3,377 |
| Chalinze Junction | 3,063 | 2,983 | 3,374 | 3,140 | 3,349 |
| Chalinze Township (Msata) | 3,067 | 2,987 | 3,378 | 3,144 | 3,354 |
| Kibiti | 3,069 | 2,989 | 3,380 | 3,146 | 3,356 |
| Kisarawe | 3,056 | 2,976 | 3,367 | 3,133 | 3,342 |
| Mkuranga | 3,058 | 2,978 | 3,369 | 3,135 | 3,345 |
| Rufiji | 3,076 | 2,996 | 3,387 | 3,153 | 3,363 |
| **Dodoma** | **3,107** | **3,027** | **3,418** | **3,184** | **3,394** |
| Bahi | 3,115 | 3,035 | 3,426 | 3,191 | 3,401 |
| Chamwino | 3,103 | 3,023 | 3,414 | 3,179 | 3,389 |
| Chemba | 3,134 | 3,054 | 3,445 | 3,211 | 3,420 |
| Kondoa | 3,140 | 3,060 | 3,451 | 3,217 | 3,427 |
| Kongwa | 3,105 | 3,025 | 3,415 | 3,181 | 3,391 |
| Mpwapwa | 3,109 | 3,029 | 3,419 | 3,185 | 3,395 |
| Mpwapwa (Chipogoro) | 3,121 | 3,041 | 3,431 | 3,197 | 3,407 |
| Mtera (Makatopora) | 3,126 | 3,046 | 3,437 | 3,203 | 3,413 |
| Mvumi | 3,114 | 3,034 | 3,425 | 3,191 | 3,401 |
| **Geita** | **3,214** | **3,134** | **3,525** | **3,291** | **3,501** |
| Bukombe | 3,203 | 3,123 | 3,514 | 3,280 | 3,490 |
| Chato | 3,235 | 3,155 | 3,546 | 3,312 | 3,522 |
| Mbogwe | 3,252 | 3,172 | 3,563 | 3,329 | 3,539 |
| Nyang'hwale | 3,229 | 3,149 | 3,540 | 3,306 | 3,516 |
| **Iringa** | **3,113** | **3,033** | **3,424** | **3,190** | **3,399** |
| Ismani | 3,118 | 3,038 | 3,429 | 3,195 | 3,405 |
| Kilolo | 3,117 | 3,037 | 3,428 | 3,194 | 3,404 |
| Mufindi (Mafinga) | 3,123 | 3,043 | 3,434 | 3,200 | 3,409 |
| Mufindi (Igowole) | 3,131 | 3,051 | 3,442 | 3,208 | 3,418 |
| **Kagera (Bukoba)** | **3,264** | **3,184** | **3,575** | **3,341** | **3,551** |
| Biharamulo | 3,239 | 3,159 | 3,549 | 3,315 | 3,525 |
| Karagwe (Kayanga) | 3,281 | 3,201 | 3,591 | 3,357 | 3,567 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 3,286 | 3,206 | 3,597 | 3,363 | 3,573 |
| Muleba | 3,264 | 3,184 | 3,575 | 3,341 | 3,551 |
| Ngara | 3,252 | 3,172 | 3,563 | 3,329 | 3,539 |
| Misenyi | 3,273 | 3,193 | 3,583 | 3,349 | 3,559 |
| **Katavi (Mpanda)** | **3,206** | **3,126** | **3,517** | **3,283** | **3,493** |
| Mlele (Inyonga) | 3,188 | 3,108 | 3,499 | 3,265 | 3,475 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 3,226 | 3,146 | 3,536 | 3,302 | 3,512 |
| Tanganyika (Ikola) | 3,224 | 3,144 | 3,535 | 3,301 | 3,511 |

217033602

# TANGAZO

| Mji | Bei ya Petroli isiyo na Ruzuku | Bei ya Petroli yenye Ruzuku | Bei ya Dizeli isiyo na Ruzuku | Bei ya Dizeli yenye Ruzuku | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kigoma** | **3,211** | **3,131** | **3,522** | **3,288** | **3,498** |
| Uvinza (Lugufu) | 3,201 | 3,121 | 3,512 | 3,278 | 3,488 |
| Muyobozi Village (Uvinza) | 3,210 | 3,130 | 3,520 | 3,286 | 3,496 |
| Ilagala Village (Uvinza) | 3,212 | 3,132 | 3,523 | 3,289 | 3,498 |
| Buhigwe | 3,209 | 3,129 | 3,519 | 3,285 | 3,495 |
| Kakonko | 3,211 | 3,131 | 3,522 | 3,288 | 3,497 |
| Kasulu | 3,220 | 3,140 | 3,531 | 3,297 | 3,507 |
| Kibondo | 3,218 | 3,138 | 3,528 | 3,294 | 3,504 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **3,119** | **3,079** | **3,382** | **3,177** | **3,409** |
| Hai (Bomang'ombe) | 3,123 | 3,083 | 3,386 | 3,180 | 3,412 |
| Mwanga | 3,112 | 3,072 | 3,375 | 3,170 | 3,402 |
| Rombo (Mkuu) | 3,136 | 3,096 | 3,399 | 3,194 | 3,430 |
| Same | 3,106 | 3,066 | 3,369 | 3,164 | 3,395 |
| Siha (Sanya Juu) | 3,126 | 3,086 | 3,389 | 3,184 | 3,415 |
| **Lindi** | **3,135** | **3,095** | **3,446** | **3,226** | **3,394** |
| Lindi-Mtama | 3,140 | 3,100 | 3,451 | 3,231 | 3,412 |
| Kilwa Masoko | 3,159 | 3,119 | 3,470 | 3,250 | 3,369 |
| Liwale | 3,171 | 3,131 | 3,482 | 3,262 | 3,415 |
| Nachingwea | 3,155 | 3,115 | 3,466 | 3,246 | 3,423 |
| Ruangwa | 3,162 | 3,122 | 3,473 | 3,253 | 3,425 |
| **Manyara (Babati)** | **3,164** | **3,124** | **3,427** | **3,222** | **3,458** |
| Hanang (Katesh) | 3,174 | 3,134 | 3,437 | 3,232 | 3,468 |
| Kiteto (Kibaya) | 3,179 | 3,139 | 3,442 | 3,237 | 3,469 |
| Mbulu | 3,177 | 3,137 | 3,439 | 3,234 | 3,470 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 3,196 | 3,156 | 3,459 | 3,254 | 3,490 |
| **Mara (Musoma)** | **3,214** | **3,134** | **3,525** | **3,291** | **3,501** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 3,227 | 3,147 | 3,538 | 3,304 | 3,514 |
| Rorya (Ingirijuu) | 3,221 | 3,141 | 3,532 | 3,298 | 3,508 |
| Rorya (Shirati) | 3,229 | 3,149 | 3,540 | 3,306 | 3,516 |
| Bunda | 3,206 | 3,126 | 3,517 | 3,283 | 3,492 |
| Bunda (Kisorya) | 3,218 | 3,138 | 3,529 | 3,295 | 3,505 |
| Butiama | 3,212 | 3,132 | 3,522 | 3,288 | 3,498 |
| Serengeti (Mugumu) | 3,223 | 3,143 | 3,534 | 3,300 | 3,509 |
| Tarime | 3,223 | 3,143 | 3,534 | 3,300 | 3,510 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 3,229 | 3,149 | 3,540 | 3,306 | 3,515 |
| **Mbeya** | **3,156** | **3,076** | **3,467** | **3,233** | **3,442** |
| Chunya | 3,165 | 3,085 | 3,476 | 3,242 | 3,452 |
| Chunya (Makongolosi) | 3,171 | 3,091 | 3,481 | 3,247 | 3,457 |
| Chunya (Lupa Tingatinga) | 3,173 | 3,093 | 3,483 | 3,249 | 3,459 |
| Kyela | 3,172 | 3,092 | 3,482 | 3,248 | 3,458 |
| Mbarali (Rujewa) | 3,140 | 3,060 | 3,451 | 3,217 | 3,426 |
| Rujewa (Madibira) | 3,153 | 3,073 | 3,464 | 3,230 | 3,440 |
| Rujewa (Kapunga) | 3,150 | 3,070 | 3,461 | 3,227 | 3,436 |
| Rungwe (Tukuyu) | 3,165 | 3,085 | 3,476 | 3,242 | 3,451 |
| **Morogoro** | **3,074** | **2,994** | **3,384** | **3,150** | **3,360** |
| Mikumi | 3,089 | 3,009 | 3,400 | 3,166 | 3,376 |
| Kilombero (Ifakara) | 3,112 | 3,032 | 3,422 | 3,188 | 3,398 |
| Kilombero (Mlimba) | 3,134 | 3,054 | 3,445 | 3,211 | 3,420 |
| Kilombero (Mngeta) | 3,123 | 3,043 | 3,434 | 3,200 | 3,410 |
| Ulanga (Mahenge) | 3,122 | 3,042 | 3,433 | 3,199 | 3,409 |
| Malinyi | 3,132 | 3,052 | 3,443 | 3,209 | 3,419 |
| Kilosa | 3,092 | 3,012 | 3,403 | 3,169 | 3,379 |
| Gairo | 3,092 | 3,012 | 3,403 | 3,169 | 3,379 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 3,084 | 3,004 | 3,395 | 3,161 | 3,371 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 3,074 | 2,994 | 3,384 | 3,150 | 3,360 |
| Turian | 3,099 | 3,019 | 3,410 | 3,176 | 3,385 |
| **Mtwara** | **3,122** | **3,082** | **3,433** | **3,213** | **3,408** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 3,159 | 3,119 | 3,469 | 3,249 | 3,457 |
| Masasi | 3,138 | 3,098 | 3,449 | 3,229 | 3,433 |
| Newala | 3,143 | 3,103 | 3,454 | 3,234 | 3,440 |
| Tandahimba | 3,136 | 3,096 | 3,447 | 3,227 | 3,433 |
| Nanyamba | 3,136 | 3,096 | 3,447 | 3,227 | 3,433 |
| **Mwanza** | **3,199** | **3,119** | **3,510** | **3,276** | **3,485** |
| Kwimba | 3,217 | 3,137 | 3,527 | 3,293 | 3,503 |
| Magu | 3,207 | 3,127 | 3,518 | 3,284 | 3,493 |
| Misungwi | 3,193 | 3,113 | 3,504 | 3,270 | 3,480 |
| Sengerema | 3,231 | 3,151 | 3,542 | 3,308 | 3,518 |
| Ukerewe | 3,258 | 3,178 | 3,569 | 3,335 | 3,545 |
| **Njombe** | **3,141** | **3,061** | **3,452** | **3,218** | **3,428** |
| Njombe (Kidegembye) | 3,162 | 3,082 | 3,473 | 3,239 | 3,448 |
| Ludewa | 3,179 | 3,099 | 3,490 | 3,256 | 3,466 |
| Makambako | 3,133 | 3,053 | 3,444 | 3,210 | 3,420 |
| Makete | 3,172 | 3,092 | 3,483 | 3,249 | 3,459 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 3,139 | 3,059 | 3,450 | 3,216 | 3,425 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **3,222** | **3,142** | **3,532** | **3,298** | **3,508** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 3,222 | 3,142 | 3,532 | 3,298 | 3,508 |
| Kalambo (Matai) | 3,229 | 3,149 | 3,540 | 3,306 | 3,515 |
| Nkasi (Namanyele) | 3,235 | 3,155 | 3,546 | 3,312 | 3,522 |
| **Ruvuma (Songea)** | **3,208** | **3,168** | **3,518** | **3,298** | **3,459** |
| Mbinga | 3,220 | 3,180 | 3,531 | 3,311 | 3,471 |
| Namtumbo | 3,199 | 3,159 | 3,509 | 3,289 | 3,464 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 3,246 | 3,206 | 3,556 | 3,336 | 3,481 |
| Tunduru | 3,173 | 3,133 | 3,484 | 3,264 | 3,438 |
| **Shinyanga** | **3,178** | **3,098** | **3,488** | **3,254** | **3,464** |
| Kahama | 3,182 | 3,102 | 3,493 | 3,259 | 3,469 |
| Kishapu | 3,186 | 3,106 | 3,496 | 3,262 | 3,472 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 3,194 | 3,114 | 3,505 | 3,271 | 3,480 |
| Ushetu (Kangeme Village) | 3,200 | 3,120 | 3,510 | 3,276 | 3,486 |
| Salawe | 3,191 | 3,111 | 3,502 | 3,268 | 3,478 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **3,196** | **3,116** | **3,506** | **3,272** | **3,482** |
| Busega (Nyashimo) | 3,208 | 3,128 | 3,518 | 3,284 | 3,494 |
| Itilima (Lagangabilili) | 3,196 | 3,116 | 3,506 | 3,272 | 3,482 |
| Maswa | 3,189 | 3,109 | 3,500 | 3,266 | 3,476 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 3,201 | 3,121 | 3,511 | 3,277 | 3,487 |
| **Singida** | **3,139** | **3,059** | **3,450** | **3,216** | **3,426** |
| Iramba | 3,152 | 3,072 | 3,462 | 3,228 | 3,438 |
| Manyoni | 3,124 | 3,044 | 3,435 | 3,201 | 3,411 |
| Itigi (Mitundu) | 3,140 | 3,060 | 3,450 | 3,216 | 3,426 |
| Ikungi | 3,135 | 3,055 | 3,446 | 3,212 | 3,421 |
| Mkalama (Nduguti) | 3,164 | 3,084 | 3,475 | 3,241 | 3,451 |
| **Songwe (Vwawa)** | **3,165** | **3,085** | **3,476** | **3,242** | **3,452** |
| Songwe (Mkwajuni) | 3,172 | 3,092 | 3,483 | 3,249 | 3,459 |
| Ileje | 3,169 | 3,089 | 3,480 | 3,246 | 3,456 |
| Momba (Chitete) | 3,174 | 3,094 | 3,485 | 3,251 | 3,461 |
| Tunduma | 3,169 | 3,089 | 3,480 | 3,246 | 3,456 |
| **Tabora** | **3,157** | **3,077** | **3,468** | **3,234** | **3,443** |
| Igunga | 3,157 | 3,077 | 3,467 | 3,233 | 3,443 |
| Kaliua | 3,170 | 3,090 | 3,481 | 3,247 | 3,457 |
| Ulyankulu | 3,167 | 3,087 | 3,478 | 3,244 | 3,454 |
| Nzega | 3,167 | 3,087 | 3,478 | 3,244 | 3,454 |
| Sikonge | 3,166 | 3,086 | 3,477 | 3,243 | 3,452 |
| Urambo | 3,167 | 3,087 | 3,478 | 3,244 | 3,453 |
| Uyui | 3,163 | 3,083 | 3,474 | 3,240 | 3,450 |
| Mpyagula | 3,189 | 3,109 | 3,499 | 3,265 | 3,475 |
| **Tanga** | **3,073** | **3,033** | **3,336** | **3,131** | **3,381** |
| Handeni | 3,094 | 3,054 | 3,357 | 3,152 | 3,361 |
| Kilindi | 3,109 | 3,069 | 3,372 | 3,167 | 3,395 |
| Korogwe | 3,085 | 3,045 | 3,348 | 3,143 | 3,374 |
| Lushoto | 3,095 | 3,055 | 3,357 | 3,152 | 3,384 |
| Mkinga (Maramba) | 3,080 | 3,040 | 3,343 | 3,138 | 3,396 |
| Muheza | 3,078 | 3,038 | 3,341 | 3,136 | 3,381 |
| Pangani | 3,080 | 3,040 | 3,343 | 3,138 | 3,388 |

**JEDWALI 4: BEI ZA JUMLA (SHS/LITA)**

| Bandari | Bei ya Petroli Isiyo na Ruzuku | Bei ya Petroli yenye Ruzuku | Bei ya Dizeli Isiyo na Ruzuku | Bei ya Dizeli yenye Ruzuku | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 2,917.46 | 2,837.46 | 3,227.34 | 2,993.34 | 3,203.11 |
| Tanga | 2,941.63 | 2,901.63 | 3,203.88 | 2,998.88 | |
| Mtwara | 2,990.46 | 2,950.46 | 3,300.40 | 3,080.40 | |

Mha. Modestus M. Lumato
**MKURUGENZI MKUU**

217033602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali ianze kukabili ughali huu wa nafaka

**BEI** za vyakula muhimu kama mchele, unga wa ngano na sembe imepaa kiasi cha kuwafanya watu hasa wa kipato kidogo kufikiria hatima yao.

Si hivyo tu, wapo wanaoingiwa na hofu zaidi kwa kuwa hata sasa wanakabiliwa na njaa kwa vile wanakula mlo mmoja tena unaopatikana kwa taabu.

Ni kweli kuwa kuna ugumu wa maisha unaotokana na sababu nyingi zikiwamo kupanda kila wakati kwa bei ya mafuta, kunakopandisha bei za kila kitu kuanzia bidhaa za viwandani, chakula hadi nauli ni mambo ambayo yanawafanya wengi kukosa utulivu, amani moyoni pamoja na matumaini.

Hivi karibuni uhaba wa mvua hasa za masika umewafanya wakulima wengi kuvuna haba lakini walaji nao kukosa chakula kwa bei nafuu sokoni na kukabiliwa na njaa .

Ni kutokana na ukame kwani mikoa mingi haikuvuna nafaka za kutosha hasa mahindi, mpunga, lakini pia maharage, kunde na mengine yanayofanana na hayo hayakupatikana kama ilivyotegemewa.

Kitisho kipya cha ongezeko la bei ya vyakula masokoni kinachoshuhudiwa sasa ni matokeo ya mambo mengi kuanzia ughali wa mafuta, ukame ulioharibu mazao, kufa mifugo lakini pia mafuriko yaliyoharibu mazao na kusababisha njaa, hivyo hakuna wa kulaumiwa moja kwa moja.

Kupanda kwa bei ya chakula na watu wengi kukosa akiba ya chakula nyumbani pia wakishindwa kukinunua sokoni inamaanisha kuwa kuna dalili za njaa ambayo ni shida kubwa ya chakula kwa jamii kubwa.

Uhaba wa chakula na kuongezeka kwa bei za vyakula unamaanisha kuwa familia nyingi zitakuwa kwenye hali ngumu hasa zile ambazo zina kipato kidogo ambao ndiyo Watanzania wengi waishia mijini na vijijini.

Njaa haina macho lakini inapotokea wanaoathirika zaidi ni watoto, wahitaji, wasiojiweza hasa kaya maskini, watoto wachanga na watoto ambao wengi ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ni mbaya zaidi.

Tunakumbusha kuwa kupanda kwa bei ya chakula kunamaanisha njaa kwenye kaya kwa vile nyingi zitakabiliwa na uhaba mkubwa wa chakula.

Aidha, pia watu hasa watoto watapata utapiamlo na hali inapokuwa mbaya wanazidi kuwa na udhaifu. Hilo linatokana na lishe duni na magonjwa nyemelezi ni rahisi kuleta vifo.

Yote hayo ni kutokana na uhaba wa chakula na ughali masokoni.

Tunaamini kuwa serikali imesikia na inaona pia, tukiamini haitachelewa kulitupia macho suala la ughali wa vyakula kwa kuwa ni tatizo kwa watu wote.

Ikumbukwe kuwa watoto kukosa chakula kutasababisha hata wengine kupata utapiamlo unaosababisha kudumaa akili kuchelewa kukua, kuwa mbumbumbu na kuongeza tena gharama za kuihudumia jamii inayoathirika.

Kukiwa na watu waliokosa vyakula au wenye njaa kunamaanisha kuwa taifa litapata tena gharama za kulisha watoto waathirika hasa wa unyafuzi, udumavu watakaolazwa mahospitalini. Kadhalika kwenye elimu litakabiliwa na kazi ya kuhudumia wenye mahitaji maalumu madarasani.


Tunaishauri serikali kuliangalia suala la ongezeko la bei ya nafaka na kuchukua hatua kwa kuwa tatizo hilo lina athari kubwa kwa Watanzania zaidi ya asilimia 90, ikimaanisha kuwa walio wengi wataumia kwa njaa iwapo hali haitadhibitiwa.

Ni ushauri wetu kwa mamlaka za chakula,wabunge na wadau wengine wa kilimo na usalama wa chakula wachukue hatua wasikae kimya, waeleze ni nini cha kufanya na hata ikibidi kuangalia uwezekano wa kutumia utaratibu wa bei elekezi.

Tunakumbusha kuwa kama ambavyo serikali ilifanya kwenye mafuta iangalie uwezekano wa kutoa ruzuku kwa wafanyabiashara wa nafaka wakiwamo wasindikaji wa mahindi na ngano lakini pia wauzaji wakuu wa mpunga ili kupunguza ukali wa tatizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wabunge mtekeleze anachoshauri Kinana

Na Sabato Kasika

**BUNGE** la Tanzania, limekuwapo tangu uhuru, wabunge pia wameendelea kuchaguliwa tangu hapo na wamewawakilisha wananchi kwa vipindi tofauti na kwa idadi inayobadilika hasa wakiongezeka kutegemea jinsi majimbo yanavyoongozwa.

Wabunge hao wamekuwa wakitekeleza wajibu wao muhimu wa kupitisha bajeti ya serikali, kutunga sheria, kuishauri na kuisimamia serikali kwa niaba ya wananchi katika masuala mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya nchi na watu wake.

Hata hivyo, inawezekana kuna sehemu wabunge hao wameshindwa kutimiza wajibu wao na sasa wanakumbushwa kurudi kwenye mstari, ili waweze kuwakilisha wapigakura wao kikamilifu.

Hilo ni kutokana na kauli ya Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana ya kuwataka wabunge na madiwani kupitia chama hicho kuwa wakali katika kuisimamia serikali ili itekeleze ahadi za miradi ya maendeleo kwa wananchi.

Anatoa kauli hiyo hivi karibuni katika mikoa ya Kanda ya Ziwa kwamba kuna baadhi ya miradi ikiwamo ya maji, tiba, elimu na miundombinu ambayo inatengewa fedha, lakini zinaelekezwa sehemu nyingine.

Makamu Mwenyekiti Kinana akajipambanua kuwa ni miongoni mwa wale wanaopenda wabunge wawe wakali kidogo kuhusu mambo ya serikali, na kwamba sio wakali kwa maana ya kuisakama serikali bali kwa kuiwajibisha na kutoa mawazo mbadala ya kuboresha maisha na hali za wapigakura ambao ni Watanzania.

Katika ufafanuzi wake, anasema chama hicho ndicho kinachokwenda kwenye uchaguzi, kuomba kura, ndicho kitakachopewa viongozi au kitakachonyimwa na sio serikali, na akwamba watendaji na watumishi wa serikali wataendelea kuwapo, huku chama kikishindwa kutokoana na wao kutotimiza wajibu.

Jambo hili la wabunge kuishauri na kuisimamia serikali, lilishawahi kuzungumzwa na mara kwa mara wanakumbushwa kuwa waamke na kujenga hoja badala ya kuwa 'mabubu', ili kutekeleza wajibu wao kikatiba.

Kwa hiyo ndani ya bunge ndipo kunapelekwa bajeti ya serikali, kunatungwa sheria na mipango ya serikali, hivyo ni vyema wakatimiza wajibu wao kwa kuhakikisha zinatungwa sheria bora kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Akapigilia msumari kwa kusema, sio vyema kwa mbunge kujipendekeza ili aonekane ana nidhamu kwenye chama au serikali, kwa kuwa kufanya hivyo hatokuwa ametimiza wajibu wake wa kuwasemea wapigakura wake, Kinana anawakumbusha viongozi hao na wawakilishi wa wananchi.

Ninadhani hayo yaliyosemwa na viongozi yanatosha kuwaamsha wabunge na kuchukua hatua za kutimiza wajibu wao bungeni kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na ustawi wa nchi.

Hadi kufikia kusema hadharani kuwa wabunge wawe wakali kidogo kwa serikali, inaonyesha kuna mahali hawajatimiza wajibu wao inavyotakiwa. Hivyo ingependeza kama watatafakari kauli hiyo na kuifanyia kazi.

Kimsingi, serikali inaongozwa na binadamu, inaweka bungeni jambo likiwa na mapungufu, hivyo ni wajibu wabunge kurekebisha penye mapungufu na si kulipitisha kama wajibu tu.

Hivyo, mjadala wenye lengo la kuboresha kwa faida ya wananchi ni suala muhimu na hali hiyo inaweza kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwa watu kuwa wabunge wamekuwa ni watu wa kukubali kila jambo.

Ninadhani jambo la muhimu kama anavyoshauri kiongozi wa chama Kinana, ni wabunge kuwa wakali kwa mambo ya wananchi, hasa wanapoona mambo yanakwenda ndivyo sivyo, kwa kujenga hoja zenye manufaa kwa umma.

# Kinana ataka viongozi ving'ang'anizi watoswe

**Na Beatrice Shayo,** MWANZA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimewataka wanachama wake kuwapiga chini viongozi ving'ang'anizi wanaotaka kubaki madarakani kwa kutumia rushwa kwenye uchaguzi unaoendelea ndani ya chama.

Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Kanali Mstaafu Abdulrahmani Kinana, alisema hayo jana wakati akizungumza na wanachama wa CCM wakati akihitimisha ziara yake katika Uwanja wa CCM Kirumba, jijini hapo baada ya kukagua miradi ya maendeleo.

Kinana, alisema kumekuwa na figisu katika uchaguzi unaoendelea ndani ya chama kwa kuwapo viongozi wanaowanunia wenzao wanaotaka kugombea huku wakitumia rushwa ili wasiondolewe.

Alisema wanachama wa CCM kuchukua fomu si dhambi bali ni haki yao ya kikatiba na hakuna mwenye hati miliki ya nafasi ya uongozi ndani ya chama hicho.

Kinana alisema utaratibu wa chama wanaochaguliwa hukaa kwa miaka mitano baada ya kumalizika nafasi zinakuwa wazi na mtu yeyote anayetaka kugombea yuko huru kufanya hivyo.

Alisema inasikitisha kuona baadhi ya viongozi walio madarakani wamekuwa wakinuna pale wanapoona mtu anataka kugombea na wengine huvunja urafiki.

"Mtu anataka kugombea akibainika anaacha urafiki siku hiyo hiyo. Kiongozi ananuna utafikiri amegongewa misumari kwenye kiti, hataki kuondoka," alisema.

"Wakati wakitafuta uongozi wamekuwa wanafanyiwa mizengwe kwa kuwakata majina yao na kusingiziwa uzushi, huku wengine wananyimwa fomu za kugombea nafasi hizo.

Sababu ni moja ubinafsi wa uongozi. Wanataka watu wao ndio wachaguliwe si watu wanavyotaka.

"Bahati nzuri mnawajua viongozi wanaotumia nafasi zao, wanaowanyima wenzao nafasi, wanaotengeza mizengwe, wanaotaka wachaguliwe watu wanaowachagua wao hawafai na mimi naomba kiongozi wa namna hiyo akifika katika uchaguzi mpigeni chini hafai," alisema.

Kinana alisema inashangaza kuona baadhi ya viongozi wanajisahau walipoingia madarakani waliwakuta wenzao, wanapoona wanaotaka kugombea kikwazo kwao, basi wawafuate na waelezane dhamira zao na si kutishana.

Pia alisema kiongozi anayetumia fedha kusaka uongozi hafai kwani wapo baadhi yao wasiokuwa nazo wanaogopa hata kuchukua fomu licha ya kuwa wana sifa. Kinana alisema wanao chukua fomu wapo baadhi yao ni watu wa ovyo na kwa vile kura huwa ni siri ni vyema wajumbe wakawakataa.



Ofisa Maendeleo ya Jamii na Mratibu wa Dawati la Jinsia Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, Clara Urassa (kulia), akizungumza katika uzinduzi wa awamu ya tano ya kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono kwa Wasichana na Wanafunzi Inawezekana', ambayo inaendeshwa na Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI). **PICHA: SABATO KASIKA**

# Matokeo sensa hadharani Oktoba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ASILIMIA 99.9 ya kaya na 99.87 ya majengo zimehesabiwa katika Sensa ya Watu na Makazi kwa mwaka 2022, huku Rais Samia Suluhu Hassan akitarajiwa kutangaza matokeo ya awali ya idadi ya watu Oktoba, mwaka huu.

Aidha, asilimia 0.07 ya vishwambi vya sensa kati ya 205,000 vimepotea, kuharibika na kuibwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kikao cha kamati ya ushauri ya kiufundi ya sensa, Kamisaa wa Sensa, Spika Mstaafu Anne Makinda, alisema sensa hiyo ilihitimishwa juzi kwa kukusanya taarifa za kidemographia, kiuchumi na mazingira.

"Kati ya majengo hayo, asilimia 100 yaliyochukuliwa taarifa yamehakikiwa anwani za makazi. Tumekamilisha awamu ya pili ya utekelezaji wa sensa sasa tumeingia awamu ya tatu ambayo ni muhimu sana na inajumuisha shughuli zote za baada ya kuhesabu watu," alisema.

Alizitaja shughuli hizo kuwa ni pamoja na uchambuzi wa taarifa za sensa, uzinduzi rasmi wa matokeo ya mwanzo ya sensa na usambazaji wa matokeo ya sensa yatatangazwa na Rais Samia.

"Taarifa ya mwanzo itahusu idadi ya watu waliohesabiwa nchi nzima na kwa jinsia zao katika ngazi zote za utawala, matokeo haya yatatolewa mwezi Oktoba, mwaka huu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

"Hatua inayofuata ni kwa ofisi hizi mbili za takwimu yaani Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na OCGS kuwahusisha wadau mbalimbali kwa pamoja kwenye mwongozo wa usambazaji na matumizi ya matokeo ya sensa kwa lengo la kupoke maoni ya kuboresha zaidi na kuhakikisha matokeo ya sensa yanatumika na vyombo vyote vya maamuzi ndani na nje ya nchi," aliongeza.

Kamisaa wa Sensa kutoka Zanzibar, Balozi Mohammed Haji Hamza, alisema sensa ya mwaka huu imefanyika kwa ufanisi mkubwa kwa kutumia Tehama na wataalam wa ndani.

Akizungumzia asilimia 0.01 ya watu ambao hawakuhesabiwa, Mtakwimu Mkuu wa serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema kwa Bara la Afrika ni ngumu kuhesabu kwa asilimia 100 na kwamba kimahesabu wamefikisha kiwango kilichotakiwa.

Kuhusu vishikwambi, Dk. Chuwa alisema kulikuwa na vishikwambi 205,000 ambapo asilimia 0.07 ndio vilipotea, kuharibika na kuibiwa wakati wa sensa hasa kwa makarani walioanza kuhesabu kwenye usiku wa sensa Agosti 23, mwaka huu.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **STICK UP AUCTION MART, SHUSHANA SERVICE COMPANY LIMITED, MASE INTERANATIONAL LIMITED, ITUHA GENERAL AUCTION MART AND BROKERS na INDEPENDENT AGENCIES & COURT BROKERS LTD** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD.** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| | NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|---|
| | SHUSHANA SERVICE COMPANY LIMITED | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | JOHANES J KANYANKOLE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KAGONDO-BUKOBA |
| 2 | ANTIDIUS A KATABALU | PAGALE LENYE MKATABA WA MAUZIANO | IZIGO-BUKOBA |
| 3 | JASSON P BISHAIJA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KEMONDO-BUKOBA |
| | INDEPENDENT AGENCIES & COURT BROKERS LTD | | |
| 4 | SHARIFA SHAFII RASHID | NYUMBA YENYE HATI MILIKI, KIWANJA NA.359, KITALU M | KANGE-KISERA-TANGA |
| 5 | MHINA H MUONDOMEO | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI, NA.209 KITALU A | PONGWE-PINGONI-TANGA |
| 6 | RAMADHANI A MFINANGA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MWANGA-MOSHI |
| 7 | PANKRAS L MASSAWE | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MAGEREZA-KARANGA |
| 8 | AMBROSIA R MUNUO | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI KIWANJA NA.16 KITALU A | SIHA-MOSHI |
| 9 | ELIMESIA JOSEPH MUNUO | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | WERUWERU-MOSHI |
| | MASE INTERNATIONAL LIMITED | | |
| 10 | JOSHUA WILSON OBONDO | TOYOTA SUCCEED YENYE NAMBA ZA USAJILI T203DKP | TARIME |
| 11 | JOSEPH CHACHA JOHN | PAGALE LENYE HATI MILIKI KIWANJA NA. 525 & 527 KITALU A | KIGARA-BUSWELU-MWANZA |
| 12 | GILIKI M SALISALI | KIWANJA CHENYE OFA KIWANJA NA.646, KITALU KK | BUGWETO-SHINYANGA |
| | STICK UP AUCTION MART | | |
| 13 | CHEKA ODO MPETE | PAGALE LENYE LESENI YA MAKAZI NA GARI AINA YA MITSUBISHI YENYE NAMBA ZA USAJILI T975 AXH | KOPOLO-IFAKARA |
| 14 | ASHURA A MPAPAI | SHAMBA EKARI KUMI LENYE LESENI YA MAKAZI | LUNGONGOLE-IFAKARA |
| 15 | RAJABU MAHAMOUD NTIBABARA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBASA-MANGUNGU-IFAKARA |
| 16 | HAWA P MASANGAWE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBIGU-IGIMA-IFAKARA |
| 17 | LEONARD L HALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI, KIWANJA NA.341 KITALU C | NDUNA-IFAKARA |
| 18 | YASINI SHABANI MARUSU | NYUMBA YA KULALA WAGENI, YENYE LESENI YA MAKAZI | JONGO-IFAKARA |
| 19 | HASSAN A KIGAILE | NYUMBA YENYE LESENI MAKAZI | MSASANI-IFAKARA |
| 20 | FAIDA LUCAS MWENDESHA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | NDUNA-IFAKARA |
| 21 | RASHID R NDOMONDO | NYUMBA YENYE LESENI MAKAZI | MANG'ULA-MWAYA-IFAKRA |
| 22 | GODFREY MATEI MWACHA | NYUMBA YA KULALA WAGENI YENYE LESENI YA MAKAZI | KIONJO-IFAKARA |
| 23 | MOSES MAGANGA SHIJA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | MKWETA-IFAKRA |
| 24 | HAWA P MASANGAWE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBINGU-IFAKARA |
| 25 | RENATUS MATHAYO MANG'ALU | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBASA-IFAKARA |
| | ITUHA GENERAL AUCTION MART AND BROKERS | | |
| 26 | EMMANUEL A MBOYA | GARI AINA YA TOYOTA MARK X YENYE NAMBA ZA USAJILI T743 CDU | MBEYA |
| 27 | EBELINO B MWALONGO | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | LYOTO-MBEYA |
| 28 | MWILE Y MWASHIBANDA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBALIZI-MBEYA |
| 29 | BURTON CHOMBE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI, KIWANJA NA.219, KITALU D | MBALIZI-MBEYA |
| 30 | JANKEN MWALENGO | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | TONYA-MBEYA |
| 31 | DAUDI MWAIBOFU | NYUMBA YENYE HATI MILIKI KIWANJA NA.444, KITALU P | ITIJI-MBEYA |
| 32 | ELIAS MWAKASEKELE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | IWINDI-VETA-MBEYA |
| 33 | AINASWE MALYA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | TAZARA-TUNDUMA-MBEYA |
| 34 | KIBADEN SANGA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | UYOLE-MBEYA |
| 35 | REHEMA NDEJE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO, MALI YA JACKSON M BUKUKU | IYELA-MBEYA |
| 36 | WITO MWANDUNGA | PAGALE LENYE MKATABA WA MAUZIANO | UYOLE-MBEYA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipwa kulingana na makubaliano ya benki na mnunuzi.Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Stick up Auction Mart**
**S.L.P Arusha**
**Namba za simu: 0786559593**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Mase international limited**
**S.L.P**
**Namba za simu; 0710885084/ 0743885084**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Independent agencies & court broker's ltd**
**S.L.P Moshi**
**Namba za simu: 0716264733**

**NA**

**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**Namba za simu: 0768790399, 0754774949**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Shushana company service**
**S.LP Bukoba limited**
**Namba za simu; 0767020699**

**NA**

217033402



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (wa tatu kushoto), akionyesha kitabu chenye kanuni na maadili ya kufanya kazi na mtoto baada ya kukizindua jijini Dar es Salaam jana. Wa tatu kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Mauaji yatikisa kila pembe

**Na Waandishi Wetu**

NI mauaji yanayoendelea kutikisa kila kukicha kwa watu kuuana na wengine kujiua.

Ripoti kutoka mikoa mbalimbali nchini kuhusu matukio yaliyotokea jana na juzi zinaeleza kuwa huko Mbeya mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Sinde jijini hapo, Faraja Kasole (16), ameuawa kwa madai ya kukatwa shoka na mwanafunzi mwenzake (jina linahifadhiwa) mwenye umri wa miaka 17 wa kidato cha tano.

Chanzo cha mauaji hayo kimedaiwa kuwa ni tamaa za kimwili baada ya mtuhumiwa kufanya jaribio la kumbaka mwanafunzi mwenzake na alipozidiwa nguvu alichukua shoka na kumpiga nalo kichwani.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alithibitisha tukio hilo ambalo kabla halijatekelezwa mtuhumiwa alifika nyumbani kwa mwanafunzi mwenzake ambaye muda huo alikuwa peke yake na kumvamia chumbani kwake kwa nia ya kumbaka na alipozidiwa nguvu ndipo alipoamua kuchukua shoka na kumpiga nalo.

Kamanda Matei alisema upelelezi wa shauri hilo unaendelea na baada ya kukamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua nyingine za kisheria.

**MOROGORO**

Watu wawili wa familia moja akiwamo bibi wa miaka 76, Kija Nkenda, wameuawa usiku wa kuamkia Septemba 5, mwaka huu wakati wakiwa wamelala nyumbani mwao katika Kijiji cha Itete wilayani Malinyi, mkoani Morogoro.

Mtoto wa marehemu, Kabula Masebu, alisema tukio hilo lilitokea usiku wakati wakijiandaa kulala na kutokea kijana mmoja aliyeingia ndani mwao akiwa ameshika panga na fimbo na kuanza kumshambulia mama yao.

Alisema dada yake mkubwa alijaribu kuingilia, lakini waliongezeka vijana wengine wawili wakiwa wameshika mapanga na fimbo na kuwashambulia ndugu zake hao na kusababisha vifo hivyo.

Alieleza kwa kuwa walikuwa wanawake peke yao walishindwa kujitetea, wakaamua kulala chini ili kunusuru maisha yao na watu hao walipomaliza kutekeleza mauaji hayo walikimbia.

Diwani wa Kata ya Itete, Anatory Libawa, alisema bibi huyo alikuwa akiishi na wajukuu ambao wote ni wa kike maeneo ya mashambani na kuwa vigumu kupata msaada kutoka kwa majirani.

Mkuu wa Wilaya ya Malinyi, Mathayo Masele, aliwataja waliopoteza maisha kuwa ni Kija Bundala Nkenda na mwanawe Magreth Mubula (58).

Alisema taarifa za uchunguzi wa awali zinaonesha mauaji hayo yamesababishwa na imani za kishirikina na ugomvi wa mali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilimu, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo na kutaja chanzo cha tukio hilo kuwa ni ugomvi wa kifamilia baada ya bibi huyo kuamua kumrithisha nyumba na shamba mwanawe wa kike ambaye naye ameuawa katika tukio hilo.

**NJOMBE**

Watu wawili wamefariki dunia akiwamo mwanamke mmoja anayekadiriwa kuwa na miaka 25 ambaye amekutwa amekatwa na kitu chenye ncha kali shingoni kijiji cha Kifanya, kitongoji cha Muungano Halmashauri ya mji wa Njombe.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kifanya, Albeto Mkalawa, aliiambia Nipashe kuwa tukio hilo lilitokea Septemba 2, saa 12 asubuhi kwenye pori lililopo kitongoji cha Muungano.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya mji Kibena, Ayubu Mtulo, alithibitisha kupokea mwili wa mwanamke huyo na jitihada za utambuzi zinaendelea.

Katika tukio lingine John Makweta (54), amefariki kwa kujikata koromeo kijiji cha Matembwe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Tukio hilo limetokea Agosti 31, wakati akipatiwa matibabu Kituo cha Afya Lupembe.

Mwenyekiti wa kijiji cha Matembwe, Jerome Lihawa, alisema Makweta alijikata koromeo na kuzunguka vilabuni huku akiwa amejifunga shuka kwenye jeraha lake.

"Wale watu pale kilabuni walipata mashaka baada ya kuona sauti yake haitoki vizuri na alipokuwa akiulizwa alikuwa na majibu tofauti kwa sababu alipokuja kwangu alisema kuna watu wamekuja na pikipiki wanamkimbiza akakimbia wakamwambia huwezi ukakimbia kwa sababu mama yako mzazi amechukua fedha kwetu wewe ni lazima ufe," alisema Lihawa.

"Alionekana kuchanganyikiwa sijui kwa sababu alikuwa amejikata mishipa, lakini ukisikia maelezo ya mama yake mzazi, anasema mtoto wake alitoka usiku saa kumi na alipomuuliza anakwenda wapi akajibu anakwenda kufua, akamwambia mbona muda sio rafiki akasema anaenda ndiyo akarudi amejichinja," alisema.

Hata hivyo, Lihawa alisema kijana huyo alikuwa na tabia ya kumpiga mama yake kwa sababu ya kutokumuwekea chakula.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamis Issah, amethibitisha kutokea kwa matukio hayo.

Kuhusu tukio la mtu aliyekutwa na majeraha sehemu ya shingoni na michubuko usoni, alisema hali hiyo iliwafanya kuamini kuwa ameuawa.

Alisema ni jambo la ajabu kuona tukio la mauaji linatokea kwenye kijiji, lakini marehemu anashindwa kutambulika na wenyeji wa eneo husika.

**MFANYABIASHARA AKAMATWA TUHUMA MAUAJI YA MKEWE**

Polisi mkoani Dodoma inamshikilia mfanyabiashara, Peter Mwakipesile, mkazi wa Chidachi mkoani hapa, kwa tuhuma za kusababisha kifo cha mke wake, Aisha Mfinangi, kutokana na madai ya kumpiga sehemu mbalimbali za mwili.

Akizungumza na Nipashe jana Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Martine Otieno, alisema taarifa za awali zinaeleza mtuhumiwa huyo na mkewe walikuwa na ugomvi.

Alisema mtuhumiwa anadaiwa kumpiga mke wake na kumsababishia majeraha na baadaye alikimbizwa katika Hospitali ya Rufani Dodoma, lakini alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu.

Alisema Polisi inaendelea na uchunguzi kwa ajili ya kubaini chanzo cha ugomvi huo.

Baadhi ya majirani ambao hawakutaka kutaja majina yao yaandikwe gazetini waliiambia Nipashe kuwa ugomvi wa wanandoa hao ulianza juzi majira ya usiku kwa kusikia kelele za Aisha kuomba msaada wa majirani wakati akipigwa na mume wake.

"Hata watoto nao walikuwa wanapiga kelele za kuomba msaada kwa majirani ili waje kumuokoa mama yao. Majirani walipofika eneo hilo walifanikiwa kuamua ugomvi huo na baadaye Aisha aliendelea kuugulia," alieleza mmoja wa majirani hao.

Walisema baada ya kumalizika kwa ugomvi huo, juzi Aisha alizidiwa, ndipo watoto wake waliwaita majirani na kumkimbiza hospitalini, lakini alifariki dunia muda mfupi.

Majirani hao walieleza kuwa Mwakipesile amekuwa na tabia ya kumpiga mke wake mara kwa mara hali iliyokuwa ikimlazimu Aisha kuondoka nyumbani.

***Imeandikwa na Grace Mwakalinga (MBEYA), Frank Kaundula (MOROGORO), Elizabeth John (NJOMBE) na Renatha Msungu (DODOMA).**

## NCCR yataka mabadiliko tozo

**Mary Geofrey**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi, kimeishauri serikali kupeleka bungeni hati ya dharura ya mabadiliko ya sheria ya fedha ili kufanya marekebisho ya tozo za miamala ya simu na benki zinazolalamikiwa.

Ushauri huo ulitolewa jana Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya NCCR-Mageuzi, Joseph Selasini, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tozo hizo.

Selasini aliitaka Kamati ya Bunge ya Bajeti na Wizara ya Fedha na Mipango, kukaa meza moja kwa ajili ya kufanyia kazi agizo la Rais Samia Suluhu Hassan. Pia aliitaka wizara kupeleka bajeti fupi bungeni na mapendekezo ya kuziba pengo la fedha zitakazokosekana baada ya tozo kuondolewa.

Aidha, aliwataka wananchi, wadau mbalimbali na wachumi, kuwasilisha mapendekezo ya nini kifanyike kwenye mabadiliko ya tozo hizo badala ya kulalamika na kukimbilia mahakamani.

"Tunawaomba wanachama wetu, wananchi na taasisi wenye mawazo wasisite kuyapeleka serikalini, tusilaumu tu wizara na serikali. Rais Samia ameshaagiza hili jambo lifanyiwe kazi hivyo wawasilishe mawazo yao kwa Waziri Dk. Nchemba," alisema,

Pia aliwashauri Watanzania wajikite zaidi kwenye kushauri badala ya kile alichoita 'kuponda' suala la tozo ili maoni yao yafanyiwe kazi kwa maslahi mapana ya taifa.

Selasini pia alishauri serikali kushirikisha sekta binafsi, vikundi vya kijamii na taasisi za kidini katika kuandaa bajeti zijazo ili kuondokana na malalamiko ya wananchi kama inavyotokea kwenye tozo.

Kuhusu tozo hizo, Selasini alisema ni mjadala uliochukua nafasi kubwa sana kwa nchi kwa sababu unagusa kila mwananchi anayetumia simu na anayehifadhi fedha benki.

Alisema wafanyakazi wanakatwa kodi ya mapato PAYE kwenye mishahara yao, makato ya benki na baadaye makato ya simu hali inayosababisha kupungua kwa kipato chao.

Alisema NCCR- Mageuzi wameona wana wajibu wa kulizungumzia jambo hilo kwa sababu linagusa Watanzania wengi na kwamba wanazungumza kuweka msimamo wao ili serikali ijue na ifanye marekebisho.

Kwa mujibu wa Selasini, lengo la serikali kuweka makato hayo ni kutafuta vyanzo vya mapato ili kupata fedha kwenye utekelezaji wa miradi lakini dhamira hiyo njema imesababisha sintofahamu kubwa.

Alisema akiwa mbunge alishuhudia mara kadhaa serikali ikiwasilisha bungeni makadirio ya kodi lakini ikawa haifanikiwi kama ilivyofikiriwa na wachumi walioishauri serikali.

"Hata hili la kodi licha ya matarajio kuwa makubwa athari zimekuwa kubwa sana kwa jamii kwa sababu wapo ambao wamepunguza matumizi ya simu na itafika wakati hata watu wataacha kutumia benki na kuficha fedha ndani," alisema.

Kiongozi huyo alisema serikali ilishapiga hatua kubwa katika matumizi ya huduma za fedha kidigitali lakini kutokana na makato yanayoendelea huenda matumizi ya huduma hizo yakashuka sana.

## Tani 1,590 za mbaazi zauzwa katika mnada

**Na Gideon Mwakanosya,**
TUNDURU

ZAIDI ya tani 1,590 za mbaazi zimenunuliwa katika mnada wa kwanza wa zao hilo Tunduru mkoani Ruvuma.

Meneja wa Ghala la Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru (TAMCU), Sarah Chorwa, alisema jana kuwa ununuzi huo wa tani 1,593 umefanyika kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS).

Alisema hayo ni mafanikio makubwa na kwamba mnada wa pili unatarajia kufanyika kesho ambapo hadi sasa tayari wana tani 135, na upokeaji wa mbaazi bado unaendelea.

"Tunatarajia hadi mwisho wa msimu huu, kufikisha zaidi ya tani 5,000 za mbaazi," alisema Chorwa.

Kwa mujibu wa Chorwa, katika msimu huu kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani, walinunua ufuta zaidi ya tani 2500.

Alisema mfumo wa stakabadhi ghalani ni mzuri na wakulima wengi wameukubali na kwamba unawarahisishia wanunuzi kupata mzigo kwa pamoja.

Meneja huyo alisema mfumo huo unawanufaisha watu mbalimbali wakiwamo wasafirishaji, makulima na mama lishe na kwamba serikali inapata mapato yake kwa urahisi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, akizungumzia mfumo huo alisema ndio mkombozi kwa wakulima kwa sababu unatoa soko la uhakika kwa wakulima huku akisema siasa zinapigwa chini kwa chini ili uonekane haufai.

Alisema, serikali ya mkoa imefanya mawasiliano na Wizara ya Kilimo kupata kibali cha kuuza mbaazi kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani na tayari mnada wa kwanza umefanyika wilayani Tunduru na wananchi wengi wamejitokeza na wanafaidika.

Kanali Thomas, alitahadharisha kuwa wafanyabiashara ambao hawawatakii mema wakulima, ndio wanaopambana kuhakikisha mfumo huo unakufa ili wao wafaidike.

Alisisitiza kuwa wafanyabiashara hao walikuwa wanawaibia wakulima kupitia pembejeo za kilimo ambapo hivi sasa Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa ruzuku ya mbolea kutoka Sh. 130,000 kwa mfuko hadi Sh. 70,000 na Sh. 50,000 kwa mfuko kutegemea na aina ya mbolea.

"Nawashauri na kuwasisitiza kuwa mfumo wa stakabadhi ghalani una faida kubwa zaidi kuliko uuzaji holela," alisema.

Baadhi ya wakulima kutoka Tunduru, Songea na Namtumbo walitoa rai kwa serikali kuhakikisha mfumo unakuwa endelevu kutokana na faida nyingi wanazopata wakulima.

Ahmed Salehe, mkulima wa Ligunga, Tunduru, alisema mfumo wa stakabadhi ghalani umeongeza usalama wa fedha za mkulima na umechangia kutoa ajira katika makundi mbalimbali.

Pia, alisema mfumo huo unatoa bei sawa kwa wakulima wote ambapo ametolea mfano kwenye mnada wa zao la mbaazi mkulima amenunua kwa kilo shilingi 800.

# Walia ukosefu magari ya taka

**Na Waandishi Wetu**

LICHA ya serikali za mitaa kuweka utaratibu wa magari ya kuzoa taka kupitia katika makazi na kufanya kazi hiyo, baadhi ya maeneo yameendelea kuwa machafu.

Nipashe, lilitembelea baadhi ya maeneo ya mkoa wa Dar es Salaam na kukuta takataka zikiwa zimetupwa maeneo ambayo si rasmi.

Wakizungumza na Nipashe wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Mtaa wa Mbezi Juu, walilalamika kutokupita kwa magari ya kuzoa taka, hali iliyosababisha mrundikano wa taka. Mkazi wa Mtaa wa Sakuveda, Medadi Mbulaji, alisema:

"Ukosefu wa gari kwa ajili ya kuzolea taka ngumu mtaani kwetu ni moja ya sababu za uchafuzi wa mazingira na utupaji hovyo wa taka. Gari la taka hakuna ndiyo maana unaona kitu kama kile pale".

Mkazi mwingine, Noshadi Kweka, alisema hali ya uchafu mtani kwao inachangiwa pia na elimu ndogo juu ya usafi wa mazingira, kutotii sheria zilizopo na usimamizi hafifu wa sheria za usafi wa mazingira.

Nipashe lilimtafuta Mwenyekiti wa Mtaa wa Sakuveda, Rehema Mwandelile, ambaye alisema:

"Barabara zipo ovyo, wenye magari wanashindwa kuja kuchukua taka, pia matatizo ya ulipaji wa pesa ya taka mkandarasi anataka Sh. 5,000 lakini wananchi wanataka kulipa Sh. 2,000.

Alisema hali hiyo imesababisha wakandarasi kukimbia kutokana na malipo kidogo, hivyo manispaa wanatafuta mkandarasi mwingine.

Nao wakazi wa Mtaa wa Mwananyamala Sindano, Kata ya Makumbusho wamelalamikia kuchelewa kwa gari la kukusanya taka hali inayosababisha harufu kwenye makazi yao, hivyo kulazimika kuzipeleka maeneo yasiyo rasmi.

Mmoja wa wakazi hao, Hadija Ally, alisema: "Mlundikano wa taka umekuwa mwingi kwa sababu gari la kubeba taka halijapita kwa miezi miwili. Hatutaki uchafu majumbani kwetu basi tunapeleka Mto Ng'ombe".

Mkazi mwingine, Teddy Charles, alisema: "Kila siku wanapita kukusanya Sh. 3,000 kwa mwezi lakini takataka hawaji kubeba tumeshachoka kukaa na taka nyumbani".

Akitoa ufafanuzi wa hali hiyo, Mwenyekiti wa Mtaa wa Mwananyamala Sindano, Selemani Mohamed, alisema:

"Ramani ya mtaani kwangu si nzuri kuruhusu gari kupita hivyo inakuwa ngumu kwa mkandarasi kupitisha gari lakini wamejitahidi japo taka ni nyingi. Ni kweli kuna kero ya takataka nawasihi wananchi kuacha tabia ya kutupa taka ovyo".

**Imeandaliwa Victoria Mgodomi, Owen Bariki (TUDARCo)**




Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa Benki ya CRDB, Bruce Mwile (wa pili kulia) akiweka taarifa zake, baada ya kuzindua mashine ya kuweka pesa, katika tawi ya benki hiyo Mlimani City, mkoani Dar es Salaam. Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Uwakala wa Kibenki wa Benki ya CRDB, Erick Willy (kulia), Kaimu Meneja wa Benki hiyo, Kanda ya Mashariki, George Yateta (wa pili kulia) na Meneja wa tawi hilo, Zaituni Manoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uharibifu miundombinu barabara wapungua

**Na Jenifer Gilla**

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS), umesema uharibifu wa miundombinu ya barabara umepungua kwa asilimia 30, kutokana na mikakati madhubuti waliyoiweka.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam, Harun Senkuku, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mafanikio walioyapata.

Haroun, alisema moja ya mikakati iliyosaidia kupunguza adha hiyo ni elimu waliyokuwa wanaitoa kwa madereva, wapita njia.

"Kwa kushirikiana na askari wa usalama barabarani tunaelimisha jamii namna ya kutunza miundombinu ya barabara na pia adhabu zinatazotolewa kwa watakaobainika kuharibu miundombinu hiyo kwa mujibu wa sheria na kanuni, na hii imesaidia sana kwa sababu hata wapita njia nao wamekuwa walinzi wakubwa wa miundombinu hii," alisema.

Alisema, pia wakala huo umekuwa ukitoa semina za uelimishaji kwa wadau wa sekta ya usafirishaji juu ya sheria mbalimbali za udhibiti uzito wa magari.

Haroun, alisema moja ya semina hiyo ilifanyika Oktoba mwaka jana iliyohusu kuwajengea uelewa wadau wa usafirishaji kutoka mikoa 12, ikiwamo Dar es Salaam, Mtwara, Morogoro, Dodoma, Njombe, Mbeya, Rukwa, Kigoma, Geita, Mwanza, Tabora, Arusha na Tanga.

Pia, alisema kuwapo kwa barabara za njia nne kumesaidia kupunguza ajali maeneo ya makutano zilizokuwa zinachangia kuathiri miundombinu hiyo, kwa kuwa sasa magari hayo yanapita kwa utaratibu mzuri bila msongamano.

Horoun, alisema pia TANROADS inajivunia kusimamia barabara zinazotumika katika shughuli za kibiashara kitaifa na kimataifa zinazochangia kuleta fursa za kiuchumi nchini na kukuza pato la taifa.

Alisema, tangu kujengwa kwa barabara hizo hakujatokea malalamiko yoyote ya kuwapo kwa matatizo katika barabara hizo kwa kuwa zimejengwa kwa ubora uliokidhi viwango vya kimataifa.

Alisema, wakala huo unaendelea kuboresha miundombinu ya barabara mijini na vijijini ili ziwe kichocheo cha uchumi na kufungua milango ya biashara kwa wananchi wa maeneo husika, hasa maeneo ambayo wananchi wake wanajishughulisha na kilimo.

# Wanusurika kusombwa na mafuriko

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WATU 20 kutoka kaya nne katika mtaa wa Mwembeni, Kata ya Igoma wilayani Nyamagana, wamenusurika kusombwa na mafuriko kutokana na mvua kubwa iliyonyesha juzi jijini humo.

Mafuriko hayo yalitokana na mvua kubwa iliyonyesha kwa takribani saa mbili na kusababisha mtaro unaoelekea makazi ya watu kujaa maji na kuyamwaga nje, hivyo kusambaa kwenye nyumba.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi hao wameeleza kuwa chanzo cha mafuriko hayo ni ujenzi wa mitaro inayoelekea katika makazi yao iliyohamishwa baada ya mwekezaji kujenga uzio katikati ya barabara.

"Mvua hii ilinyesha kwa muda wa saa mbili tu, lakini imesababisha madhara makubwa kama mifugo kufa, bidhaa za ndani zote zimejaa maji na kuharibika kwa vitu kama Tv, redio pamoja na vyakula vyote vimezama kwenye maji, " alisema Irene Mushi.

"Maji yamefurika katika nyumba zetu tulikuwa tumelala pamoja na watoto kidogo wapoteze maisha, lakini tumefanikiwa kuwaokoa na kuwapeleka kwa majirani," alisema Japheth Burugu.

Elizabeth Makila ambaye ni mjumbe wa nyumba 10 eneo hilo, alisema mafuriko hayo yanasababishwa na mtaro uliohamishwa kutokana na mwekezaji kuziba barabara ya mtaa huo.

Makila alisema wamefuatilia tatizo hilo bila mafanikio na kwamba bado wapo katika hatari ya kukumbwa tena na janga hilo endapo mvua zitanyesha.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Mwembeni, Mashiku Lukas, alisema tatizo hilo amekuwa akiliripoti katika mamlaka bila mafanikio yoyote.

Diwani wa Igoma, Mussa Ngolo, alisema katika juhudi za awali tayari amewasiliana Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), ili kuwasaidia kwa kupanua mtaro kubadilisha mwelekeo wa maji.

Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Mwanza anayeshughulikia miundombinu, Chagu Nghoma, alisema eneo hilo lilikuwa la mwekezaji na kwamba mtaro huo ulijengwa kwa kufuata sheria.

Alisema eneo hilo lilikuwa mali ya Jiji la Mwanza na kwamba mwekezaji huyo aliingia makubaliano na serikali ili alitumie kwa ajili ya biashara.

Aliahidi kushughulikia sakata hilo ikiwamo kujenga mtaro mwingine ili kubadilisha mwelekeo wa maji ambayo yanaenda katika makazi ya watu.



Mkandarasi akiendelea na kazi ya kutoa mchanga kwenye Mto Ng'ombe eneo la Tandale mkoani Dar es Salaam jana, baada ya ujenzi wa kuta za kingo za mto huo. **PICHA: VICTORIA MGODOMI, TUDARCo**

# Wanafunzi vyuo vikuu watakiwa kujiendeleza

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI wa Masuala ya Ushirikiano Vodacom, Rosalynn Mworia, amesema kuna haja kwa wahitimu wa vyuo vikuu nchini kujiendeleza katika programu ya Niwezeshe Fellowship, inayojihusisha na utoaji wa elimu ya uchunguzi na ushauri kupitia shirika lisilo la kiserikali Doyenne.

Mworia aliyasema hayo hivi karibuni jijini Dar es Salaam wakati wa mahafali ya kwanza ya shirika hilo na kushuhudia wanafunzi tisa wa vyuo vinane kuhusu uongozi na ushauri.

Alisema mafunzo waliyoyapata yataenda kusaidia kudumisha usawa wa kijinsia katika jamii kupata viongozi bora na wenye uthubutu.

"Niwapongeze wahitimu wote tisa waliohitimu na kumaliza kozi yao ya mwaka mmoja kwa mwaka 2021. Wote mmebahatika kupata elimu thabiti ya uongozi. Huu ni mwanzo wa kuwa na viongozi bora wanawake duniani kote.

"Inafahamika kuna pengo kubwa la usawa wa kijinsia katika uongozi nchini Tanzania na duniani, inasikitisha sana kuona wanawake wana nia ya kuifikia nafasi fulani lakini wanakosa uwezo au uthubutu," alisema.

Mwakilishi wa Ubalozi wa Uholanzi, Jay Piare, ambao pia ni wafadhili wa mradi huo kwa mwaka huu, alisema ubalozi ulivutiwa na mradi huo na kuamua kuufadhiri kama sehemu ya kuunga mkono jitihada hizo.

"Huu ni mfano wa kuigwa na wenye ushawishi kwa wanafunzi wenzao katika vyuo vikuu ulimwenguni katika kufikia usawa wa kijinsia, kwa bahati nzuri sera ya kimataifa ya Uholanzi, kuhusu haki za wanawake na usawa wa kijinsia.

"Nchi hiyo inachangia katika kufikia malengo endelevu ya milenia (SDGs), hususan lengo la tani linalozungumzia usawa wa kijinsia na uwezeshwaji wa wanawake na wasichana kwa lengo la kuongeza viongozi wanawake kwenye ngazi za maamuzi," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Doyenne, Fatma Kauga, alisema lengo programu ya Niongoze Fellowship ni kuwalea viongozi wa kike ambao watachukuliwa kutoka vyuo vikuu.

"Ni programu ya kwanza kabisa ya uongozi kwa wanafunzi wa kike kutokea nchini kwa vyuo vikuu na sekondari lengo letu ni kutengeneza fursa ya kipekee kwa wasichana kukuza ujuzi wao katika uongozi wakati wakiendelea kupata mafunzo ya kitaaluma kupitia programu mbalimbali," alisema.

Mmoja wa wahitimu, Barbara Malata, alishukuru kupatiwa mafunzo hayo akibainisha kuwa yamebadilisha maisha yake na kumpa uzoefu mpya.

"Ninayo furaha kubwa sana na najivunia kwa mafanikio, haya, ni mafunzo yaliyobadilisha maisha yangu kwa namna moja au nyingine kwani programu hii ya mwaka mzima haikutupa tuu uzoefu mpya, au kuboresha ujuzi wa uongozi unaohitajika ili kufikia maendeleo ya kimataifa pia umetusaidia katika kukabiliana na vikwazo katika safari yetu ya uongozi tunashukuru sana kwa nafasi hii," alisema.

# Mkataba kuongeza uzalishaji mbegu wasainiwa

**Na Renatha Msungu**

WAKALA wa Mbegu za Kilimo (ASA) umetiliana saini mkataba na Kampuni ya Pro Agro Global Ltd, wenye thamani ya Sh. bilioni 18 kwa ajili ya kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya Msimba, Arusha na Kilimi.

Mkataba huo unalenga kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwenye zaidi ya hekta 800.

Akizungumza baada ya hafla fupi ya kutia saini mkataba huo, iliyofanyika makao makuu ya ASA, Mtendaji Mkuu wa ASA, Dk. Sophia Kashenge, alisema mkataba huo ni utekelezaji wa maelekezo ya Wizara ya Kilimo wa kuhakikisha uzalishaji wa mbegu bora za kilimo unakuwa wa uhakika usiotegemea mvua.

Dk. Kashenge alisema mashamba yatakayopitiwa na mradi huo Mashamba Kilosa mkoani Morogoro lenye ekari 500, Ngaramtoni Arusha ekari 500 na Kilimi, Nzega mkoani Tabora lenye ukubwa wa ekari 1,000.

Alisema ufungaji wa miundombinu hiyo utaongeza uzalishaji wa mbegu kwa msimu mzima wa mwaka, tofauti na sasa ambapo mashamba yote huzalisha mbegu wakati wa mvua pekee.

Mtendaji Mkuu huyo alisema utekelezaji wa mradi huo unaanza sasa na muda wa kukamilika uwekaji wa miundombinu hiyo hautazidi miezi 10 kama mkataba unavyosema.

Alisema katika mkataba huo, kuna baadhi ya maeneo yatachimbwa visima na mabwawa na shamba la Msimba ni uchimbaji wa visima na bwawa, wakati Ngaramtoni ni uchimbaji wa visima na bwawa pia. Shamba la Kilimi likiwekewa miundombinu ya umwagiliaji kutokana na uwapo wa bwawa la Kilimi lenye maji ya kutosha.

Dk. Kashenge aliishukuru serikali kwa kuwa na kiu kubwa ya mabadiliko ya kilimo kutoka kilimo cha kutegemea mvua hadi kilimo cha umwagiliaji.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Pro Agro Global Ltd ya Arusha, Bryson Maro, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuziamini kampuni za wazawa kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ambazo awali zilikuwa haziaminiki.

Alisema kulingana na mkataba, kazi hiyo itaanza mara moja ili kuhakikisha kila kitu kinakwenda kama kilivyopangwa ndani ya mkataba huo.


**USAWA KIJINSIA**

Wanaharakati usawa kijinsia wawaambia wanahabari bebeni bango tufike 50/50

Ukurasa 12



Ukurasa 13



**AKIWAHAKIKISHIA AMANI NA HESHIMA ... Mteule Ruto kwenye salamu zenye vichekesho, vijembe kwa rafiki Kenyatta, mshindani Odinga**



# Ukimya uchaguzi viongozi CCM unavyoakisi zama mpya kisiasa

**Na Ani Jozeni**

UCHAGUZI ndani ya CCM miaka iliyopita ulikuwa wenye ushawishi mkubwa na kampeni za wazi, lakini mwaka huu shughuli hiyo inaendelea bila dalili za wazi kuwa chama tawala kiko katika mchakato wa kuchagua safu zake za uongozi.

Hali hiyo inaendana na kupungua kwa ushawishi wa makundi ya watia nia na wasaidizi wao au wapambe wao kutokana na kupungua siyo tu kwa mahitaji ya wananchi kwa watia nia kama hao kuleta majibu kwa masuala yanayowasumbua.

Ni hata pia kushuka uwezo wao kuinua hisia hizo kwa kutoa motisha wafanye kampeni. Huenda ni mwendelezo wa taratibu za uchaguzi za awamu ya tano.

Wengi wanaweza kuhisi kuna aina ya mdororo wa uchaguzi na kampeni katika mazingira kama haya, watu kuingia katika mzunguko wa uchaguzi kama vile ni kutimiza wajibu na watiania kujikagua mara kadhaa kama inafaa wajitumbukize huko au waache.

Katika mazingira kama hayo watiania pia wanabadilika, kuna mchujo wa kimawazo na uchangamfu wa ushindani ambao unaweza kuwapangua ambao hawahitaji nafasi hizo ili kupanda kimaisha, mithili ya mtu anayepata kazi kubwa zaidi ya ile anayoifanya.

Ni tofauti na mtu anayeridhika na kazi yake ila anataka sifa zaidi. Kuna aina nyingine ya wagombea ambao walikuwa wanaleta shamrashamra za kila aina awali, na ndiyo ambao ushiriki wao ulianza kudorora au kuyeyuka wakati wa awamu ya tano, kwani unaweza kusema iliundwa aina 'jamhuri ya kimapinduzi'.

Kielelezo chake kimojawapo ni uwazi wa kiimla, au 'democratic centralism,' ambako takriban kila kitu kinawekwa hadharani, madudu ya watendaji yakianikwa na kila mtu anajua kwanini hatua mbalimbali au maamuzi yamefanyika na kwa wakati ule.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara Abdulrahman Kinana. **PICHA: MAKTABA ,**

Ndiyo hali iliyojengeka kipindi kilichopita, suala la msingi hapa ni kuwa hali hiyo ipo bado. Lakini wapo wanaotaka kuwapo kwa uwazi wa kidemokrasia (liberalism) ili vizuizi vyote vya kisiasa viwekwe pembeni, watu washiriki siasa watakavyo.

Ni jambo ambalo inaelekea linaungwa mkono kiasi fulani na Mwenyekiti wa CCM Rais wa Jamhuri ya Muungano, Samia Suluhu Hassan.

Ila jitihada za Rais Samia kusimamia utawala wa haki mara nyingi zinawapa silaha au nyenzo wanaopingana na uongozi wake kwani itikadi yao hasa ni upinzani.

Ndiyo maana kundi hilo la wanaharakati wa uhuru wamefurahia sana Rais Samia kuwakemea polisi kuhusu kukamata watuhumiwa bila kufanya upelelezi unaotosha mshukiwa kupelekwa mahahakamani.

Wametaka kuwe na chombo maalum cha kusimamia utendaji Jeshi la Polisi ili watangulize haki.

Ni jambo ambalo lina mchongo wa kisiasa vile vile, kwani kuzuia watu wasikamatwe ovyo kwa kutuhumiwa makosa ya jinai ni ngazi ya juu kiitikadi ya kufanya kazi kwa kufuata sheria na katiba na kwa njia hiyo itakuwa ni jambo lisiloingia akilini kuwa mtuhumiwa wa jinai hakamatwi ovyo, ila mshiriki kisiasa abughudhiwe kwa urahisi.

Hivyo ukisikia watu wanababujikwa na machozi watuhumiwa wa ujambazi kukaa miaka bila kesi kusikilizwa au kumalizika, usidhani kuwa wanawataka warudi mitaani, la hasha. Kuna mchongo wa kisiasa wa kupanuliwa uhuru.

Ndiyo maana uchaguzi wa sasa ndani ya CCM unakuwa na sura tofauti, lakini suala tangulizi siyo haya mabadiliko ya kutaka uwazi na ukweli zaidi, au uhuru mpana zaidi katika vyombo vya habari, kwani hadi sasa bado hizo ni nia chanya zinazoelezewa na Mwenyekiti wa CCM.

Bado hakuna uhakika kuwa, nje ya uwazi zaidi kiasi fulani katika utoaji na usambazaji wa habari, hali itakuwaje katika siasa, kwani upo mtindo mpya wa kuendesha siasa ambao ulishazoeleka, uliosahihisha bashasha na nderemo za nyakati zilizopita.

Suala hapa ni jinsi ya kujaza pengo hilo la uchangamfu, au labda ni vyema hali ibaki hivyo ilivyo ili wasizuke watu wakawa juu ya chama, majina yao yasipopita kuwe na hali ya hatari.

Na pia ilifikia mahali hata chama chenyewe kinashindwa kuwa na uwezo wa kusimamia ipasavyo mtiririko wa kutiania (kuchukua fomu kuchaguliwa) halafu suala hilo lifike ngazi za juu.

Badala ya kupeleka majina yote Kamati Kuu halafu waondoe yeyote ambaye chama hakina imani naye, mchujo ufanywe na Halmashauri Kuu na kura ipigwe na Mkutano Mkuu, kanuni zikabadilishwa 2012.

Ikaunda Kamati Maalum ya Mchujo, orodha yake ikapitishwa kwa taabu na Kamati Kuu na wajumbe Halmashauri Kuu wakaimba mbele ya Mwenyekiti na Katibu Mkuu kuwa wana imani na mgombea fulani katika wakati huo!

Tangu wakati huo ni miaka saba imepita na kutokana na mabadiliko yaliyofuatia, hasa serikalini na uongozi wa mashirika ya umma au mamlaka za sekta tofauti, si rahisi kusema kuwa bado wapo watu 'wenye nguvu' za kutingisha chama kama wakati ule.

Na pia hakuna dhamira zilizojichimbia za kurithishana uongozi kwa ajili ya maslahi ambayo haikuwa rahisi kuyaficha, kumpa uwezo mwenyekiti kuongoza kamati ya mchujo, ubunifu wa kitaasisi ulioondoa uwazi na demokrasia katika chama.

WADAI HAKI YAO KATIKA SIASA

# Wanaharakati usawa kijinsia wawaambia wanahabari bebeni bango tufike 50/50

**Na Sabato Kasika**



Mtaalam wa habari, Alakok Mayombo (kulia), akisisitiza jambo katika mafunzo ya uandishi wa taarifa za kuhamasisha usawa wa kijinsia kwa wanahabari.

MWAMKO wa wanawake katika siasa na ngazi za maamuzi, unaelezwa kuwa bado ni mdogo, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo baadhi ya jamii kukumbatia mila na desturi ambazo zimepitwa na wakati.

Hivyo, waandishi wa habari wanakumbushwa kuwa hawana budi kutumia vitendea kazi vyao kufikisha ujumbe kwa jamii utakaosaidia kubadili baadhi ya mila na desturi zilizopitwa na wakati, ili kuondoa mfumo dume unaokwamisha kufikia maelengo ya uwiano sawa wa wanawake na wanaume wa 50/50.

Inaelezwa kuwa dunia kwa sasa inaendelea kusonga mbele katika mchakato wa kufikia lengo la usawa, katika jamii na hata kwenye ngazi za maamuzi, na kwamba ni muhimu waandishi kusaidia kuhamasisha usawa huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi isiyo la kiserikali inayoshughulikia kubadili maisha ya wanawake, vijana na watoto iitwayo TIBA, Marcela Lungu, ndiye anayesema hayo, katika mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kitaaluma wanahabari kuhusu masuala la jinsia.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na taasisi ya Internews Tanzania, ambapo anasisitiza suala la uongozi katika jicho la kijinsia kwa ajili ya kuongeza sauti za wanawake katika ngazi ya maamuzi.

### JICHO LA JINSIA

Marcela anasema, uongozi katika jicho la jinsia ni dhana pana inayolenga kuongeza ushiriki wa wanawake, ili kuwa na uwiano wa sauti au uwakilishi unaolingana katika siasa na ngazi za kufanya maamuzi.

"Ni muhimu waandishi mjue ni kwa nini tunaangalia uongozi katika jicho la jinsia, kwani ni dhana pana ya unawakilisha makundi mbalimbali hivyo ni vyema kuweka uwiano ili kuwa na uwakilishi mpana," anasema Marcela

Anasema majukumu ya kijinsia huwa yanatengezwa na jamii, mitazamo, akitolea mfano kwamba kazi ya kupika au kufua hujulikana kama ya mwanamke na kazi ya kulima kuwa ya mwanaume.

"Lakini ukweli nikwambaa, mwanaume anaweza kupika au kufua siyo na pia mwanamke anaweza kulima, hivyo, dhana ni vyema jamii ikaondokana na mtindo wa kutengeneza majukumu ya kijinsia," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema mtindo huo ndio umesababisha baadhi ya wanawake kushindwa kushiriki katika siasa na ngazi nyingine za maamuzi, wakiamini kuwa nafasi hizo ni za wanaume.

"Ni muhimu waandishi mtumie kalamu zenu kuelimisha umma kuelewa muhimu wa uongozi katika jicho la jinsia ili, jamii iachane na mtindo huo kwa kutambua kuwa jinsia ni mgawanyiko wa majukumu," anasema.

Anasema waandishi wa habari wakitumia kalamu zao kuhamasisha uswa wa kijinsia, watakuwa wamesaidia juhudi zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan za kuendelea kutafuta asilimia 50 kwa 50.

### NI KWA WOTE

Ofisa Mradi Mwandamizi wa Internews, Victoria Rowan anasema ni muhimu wanahabari kuelimisha umma kuwa suala la kutafuta usawa wa kijinsia, halihusu wanawake pekee bali wanaume pia wamo.

"Usawa wa kijinsia ni sawa na mwanamke ni mwanamke ila suala la uongozi linahusu akili na uwezo wa kuongoza, hivyo halibagui jinsi, hivyo ni muhimu waandishi kulitambua hilo," anasema Victoria.

Anasema kumekuwapo na kutojua usawa wa kijinsia, na kwamba taasisi inaweza ikamuomba mhariri kutuma mwandishi kushirikia mafunzo kuhusu usawa huo na kujibiwa kuwa hayo ni ya waandishi wa kike.

Mtaalam wa msuala ya habari wa taasisi hiyo, Alakok Mayombo anasema, wamekuwa wakitoa mafunzo kwa waandishi wa habari ili waandike habari zinazoleta mabadiliko katika jamii.

"Njia mojawapo ya kufikia usawa wa huo ni mafunzo kama haya, lakini pia tumekuwa tukijitahidi kuongelea kuwapo kwa sera inayosimamia masuala ya jinsia katika vyombo vya habari ili sauti za wanawake zisikike katika vyombo hivyo," anasema Alakok.

Anasema, kupitia kalamu, waandishi wanaweza kubadilisha mfumo na kuwapo waandishi wanawake ambao ni kutolea mfano katika kazi zao, kushiriki kuandaa habari zinazozalisha viongozi wengi wanawake.

"Siyo kuandika stori za wanawake kupigwa au kubakwa tu, kwani hizo zinaelekeza mamlaka kuchukua hatua, lakini tunataka kuhakikisha wanawake wanapanda juu wengine kuwa tayari kupanda juu," anasema.

### MTAZAMO HASI

Mhadhiri Msaidizi wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (SJMC), Zuhura Seleman, anaeleza kuwapo na mtazamo hasi kwamba wanaume wana akili kuliko wanawake.

"Jamii inatakiwa kuachana na mtazamo huo, na nyie waandishi mna kazi ya kutumia kalamu zenu kuitoa katika mtazamo huo ambao ni wazi unamkandamiza mwanamke," anasema Zuhura.

Anaongeza kuwa, waandishi pia wanatakiwa kuwa jicho la usawa wa kijinsia kila habari wanazoandika na kuangalia mambo ya sera, bajeti na afya kama kuna usawa huo.

Zuhura anasema wanatakiwa kuhesabu idadi ya viongozi na kuona kama kuna uwiano, iwapo iddai ya wanaume itakuwa kubwa, basi wahoji hali hiyo kwa ajili ya kuhamasisha usawa wa kijinsia.

"Kumekuwapo na mtazamo hasi kwamba wanaume wana akili kuliko wanawake. Msaidie jamii kuachana na dhana hiyo ambayo haina ukweli na unalenga kumkandamiza mwanamke," anasema.

Anakumbushia stori aliowahi kusoma katika gazeti la Kiswahili ikimuelezea mwanamke aliyeingia kwenye siasa ikimtaja kama mtaalum wa kukaanga chapati badala ya kumuelezea kama mwaansiasa au kiongozi.

Mkuu wa Miradi asasi ya kiraia ya C-SEMA, Michael Marwa, anasema vyombo vya habari vina uwezo wa kuchochea usawa wa kijinsia katika jamii na kubadili mtazamo kuhusu usawa.



Mhadhiri Zuhura Seleman (kushoto) kutoka Shule Kuu ya Uandishi wa Habari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (SJMC), akiwasilisha mada **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

AKIWAHAKIKISHIA AMANI NA HESHIMA ...

# Mteule Ruto kwenye salamu zenye vichekesho, vijembe kwa rafiki Kenyatta, mshindani Odinga

**Na Gaudensia Mngumi**

JUMANNE ijayo, Septemba 13 itakuwa shangwe kuu kwa Wakenya ambao jibu lao 'limetiki' na kisiasa kwenye uchaguzi. Leo hii zimebakia siku sita ufike wakati, Rais Mteule William Ruto kula kiapo cha kuliongoza taifa hilo.

Hapo anahama kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais aliyoikalia kwa miaka 10 na kuingia ofisi ya Rais.

Ni baada ya Mahakama ya Juu zaidi ya Kenya, kutupilia mbali kesi ya kupinga ushindi wa Ruto, iliyofikishwa mahakamani hapo na mpinzani wake mkuu Raila Odinga na kumtangaza Ruto kuwa ndiye mshindi anayekuwa Rais wa tano wa Kenya.

Ilichukua saa moja na nusu tu, majira ya mchana, baada ya kutolewa hukumu hiyo, Ruto analihutubia taifa nyumbani kwake Karen jijini Nairobi na kuahidi kuunda serikali kwa ajili ya Wakenya wote, akiwaambia anarejea kazini mara moja atakapoapishwa Jumanne, Septemba 13.

Katika hotuba yake ya kwanza, mara zote amaetawaliwa na tabasamu na mbwembwe za jukwaani majira ya alasiri, baada ya hukumu kutimu saa 735 mchana, anaahidi serikali kujenmga iliyo wazi ambayo, akifafanua itakomesha matumizi ya mfumo wa haki za jinai kwa sababu za kisiasa.

Katika hotuba hiyo ya aina yake anasema mashujaa ni majaji saba wa Mahakama ya Juu waliodumisha ushindi wake kwa kauli moja.

Ruto ambaye sasa ni msomi wa shahada ya juu, ngazi ya daktari wa falsafa, ambaye alipingana na kampeni iliyoongozwa na Rais Uhuru Kenyatta wake ambaye alimuunga mkono mgombea wa upinzani kutoka Muungano wa Azimio la Umoja One Kenya, Raila Odinga.

Anaahidi kukomesha visa vya watumishi wa umma kuegemea upande mmoja katika kampeni, akirejea mawaziri waliokuwa wakimuunga mkono Raila Odinga na kumkwamisha yeye.

Mawaziri hao watakaokuwa kikaangoni ni Fred Matiangi wa Mambo ya Ndani, Peter Munya (Kilimo), Eugene Wamalwa (Ulinzi), Joe Mucheru na Waziri wa Usalama wa Ndani Karanja Kibicho, ambao wanadiwa wakati wa kampeni walimuunga mkono waziwazi Odinga. Mteule Ruto, ameahidi kula nao sahani moja kwa kuleta mabadiliko bila shaka kwenye sheria.

Kiongozi huyo anasherehekea kuwapiga chini wagombea watatu, Odinga, Profesa George Wajackoyah na David Waihiga Mwaure, akipuuza hadharani mikakati ya kushikana mikono na kiongozi wa Azimio Raila Odinga, iliyoanzishwa na Uhuru Kenyatta.

Anasisitiza kwamba, Odinga inapendeza akisalia kuwa upinzani ili kuangalia na kukosoa serikali yake na kwamba hakuna tena habari za kushikana mikono kwenye awamu yake.

"Demokrasia inatarajiwa kutuunganisha watu wote, kuimarisha jamii zetu na kuboresha taasisi zake na haipaswi kuwa biashara ya chuki, hofu na kukata tamaa. Tulitoa maono na njia mbadala na tukakubalika kwa uamuzi huru wa raia wa Kenya.

'Wanasiasa sisi ni washindani tu, sio maadui. Tulishindana kuungana na kuimarisha Kenya, sio kuigawanya na kuidhoofisha nchi yetu," Ruto anasema akiwalenga Odinga na wapinzani wake wengine.

Rais Mteule anawapigia saluti majaji wa Mahakama ya Juu, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo (IEBC), huku akiwapigia makofi wanasheria wa upande wake, akisema mbele yao lipo taifa lililokuwa limechangamka na mabegani mwake alichomoka rais, akisema hao ndiyo mashujaa wa kura za ushindi.

"Shujaa wa kampeni yetu ni mama mboga na bodaboda. Shujaa wa uchaguzi huo ni Mwenyekiti Wafula Chebukati na IEBC. Shujaa wa demokrasia yetu, utawala wa sheria na utii wa katiba ni Mahakama ya Juu," anasema Dk. Ruto.

Akizungumzia ushindi wake anasema: "Uchaguzi wangu unathibitisha kwamba inawezekana kuzishinda na kupanda juu ya changamoto ulizopitia, umaskini malezi yako, hali ya kiuchumi na hata hadhi yako kwenye kijamii hadi kiwango cha juu zaidi na kufikia uongozi wa juu wa nchi hii kubwa."



Rais Uhuru Kenyatta na mgombea mwenza William Ruto (kulia), ambaye kikatiba akawa Makamu wa Rais. Wiki ijayo Uhuru anastaafu rasmi, akimauachia kiti Ruto kutawala,wakiwa ni wapinzani katika uchaguzi uliopita. **PICHA: MTANDAO.**

### AMSALIMU ODINGA

Anasema kwa Odinga, ambaye bila shaka alihama kutoka kuwa kiongozi wa upinzani hadi mtu wa pili mwenye nguvu zaidi serikalini baada ya kupeana mikono na Rais Kenyatta, Machi 2018, ni vyema abakie mwaminifu kwa roho ya upinzani.

"Tutakuwa na upinzani nchini Kenya. Hatutakuwa na kupeana mkono kama tulivyofanya hapo awali, hali iliyounda serikali ambayo hakuna aliyejua mpaka wake uko wapi.

"Ninaamini katika utawala wa sheria. Siamini katika hadithi za kupeana mikono mimi. Ninaamini katika serikali inayowajibika inayowajibishwa na upinzani unaowajibika. Hivyo ndivyo Kenya itakavyosonga mbele," anasema Dk. Ruto.

### KUMNUNIA KENYATTA

Akizungumzia jinsi 'alivyomchunia' Kenyatta anasema ili kuthibitisha ukubwa wa tatizo la kuvunjika uhusiano kati yake na Rais Kenyatta, Dk. Ruto anasema hakuwahi kuzungumza na bosi wake "kwa miezi kadhaa", huku mkuu wa nchi akiwa hajampongeza Naibu Rais wake tangu atangazwe kuwa ameshinda Agosti 15, na hata jana baada ya Mahakama ya Juu kumpa ushindi.

"Wakati wowote nitampigia simu rafiki yangu mpendwa Rais Uhuru Kenyatta ambaye sijazungumza naye kwa miezi kadhaa.

"Ninataka tufanye mazungumzo kuhusu mchakato wa kuandaa utaratibu wa kuachiana madaraka. Najua alifanya kazi kwa bidii, lakini watu wa Kenya wamefanya uamuzi wao," anasema mteule Ruto.

Anaongeza: "Nilipochagua kumuunga mkono Kenyatta, sikumpa masharti. Sijaona kosa nilipoamua kumuunga mkono mtu mwingine. Tutabaki kuwa marafiki katika muktadha wa mahali tulipo.

'Tunatazamia kujenga uhusiano katika msingi ambao tayari tunao. Kuna mambo mengi tulitaka kufanya pamoja lakini hatukufanya. Tutakamilisha miradi yote ambayo hatukuwa tumekamilisha wakati wa awamu yake."

### KENYATTA HATAGUSWA

Rais mteule Ruto ameahidi kuwa Mkuu wa Nchi Kenyatta atapewa heshima zote anastaafu kwa amani na furaha.

"Utawala wangu unatambua na kuendeleza kwa ukamilifu utamaduni ulioanzishwa wa kuwaheshimu viongozi wetu ambao wametumikia taifa hili na hautaingilia kwa namna yoyote ile marupurupu na stahili zao nyingine wanapostaafu. Ni wazee wa taifa letu wanaostahili heshima kila wakati," anasema.

Katika hotuba yake ya juzi jioni, Rais Kenyatta, anaahidi mabadiliko na mchakato wa kukabidhiana uongozi utafanyika kwa uhakika na kusema anaheshimu uamuzi wa Mahakama ya Juu ya Kenya.

"Mchakato wa kukabidhiana madaraka unaendelea. Ni nia yangu kusimamia mabadiliko ya kiutawala yanayofuata maagizo yote ya kikatiba na kuwezesha mchakato huo... napenda kuwatakia kila la kheri wote walioshinda huku wakiiongoza nchi yetu katika siku zijazo na nawashukuru wote kwa nafasi ya kulihudumia na kulitumikia taifa," anasema.

Rais Kenyatta katika hotuba yake iliyorekodiwa na kurushwa kwenye mtandao wa kijamii wa Ikulu dakika chache baada ya saa moja usiku.

# Hawa ndiyo wakongwe wanaodumu wakitumika kwenye ikulu za Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

AFRIKA Kusini ya Jangwa la Sahara ni makao makuu ya viongozi au maraisi waliotawala kwa muda mrefu zaidi duniani. Watetezi wa demokrasia wakati fulani walijaribu na wakafaulu kuwazuia marais kuongeza miongo mingi lakini mwelekeo wa uongozi wa kimabavu bado upo na unaweza kuwa unaongezeka.

Tangu mwaka wa 1960, wakuu wa nchi kadhaa katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara wamekaa madarakani kwa zaidi ya miaka 30, lakini pia vipo vyama ambavyo vimeendelea kutikisa kwa kutawala kwa miongo mingi.

**EQUATORIAL GUINEA** ndiko kuna kigogo namba moja kuishi madarakani ni Teodoro Obiang, yupo tangu mwaka 1979 hadi sasa. Mkongwe huyo mwenye miaka 77, alichukua nchi katika mapinduzi yaliyofanyika 1979 , akimpokonya madaraka mjomba wake, ambaye baadaye aliuawa kwa kupigwa risasi.

Ameshikilia uongozi tangu wakati huo, akidaiwa anawakandamiza wapinzani wa kisiasa na kuendelea kunufaika na mapato kutoka kwa hifadhi ya mafuta ambayo taifa hilo limebarikiwa.

**CAMEROON** ni namba mbili yupo Paulo Biya, anayeongoza tangu 1982, hadi sasa. Biya mwenye miaka 87, alichukua hatamu mwaka 1982 kutoka kwa Rais Ahmadou Ahidjo na ameshinda msururu wa uchaguzi, na hivi majuzi mwaka 2018 aliibuka kidedea katika kinyang'anyiro ambacho wapinzani wake walikitaja kuwa ni udanganyifu.

**JAMHURI YA CONGO**, Denis Sassou Nguesso, ni namba tatu ni mzee mkongwe ameishi madarakani kuanzia 1979-92, 1997 hadi sasa.

Sassou Nguesso (76), alishika wadhifa huo mwaka wa 1979 kabla ya kushindwa katika uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi nchini humo mwaka wa 1992.

Alipata tena mamlaka mwaka 1997 baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa muda mfupi na akabadilisha katiba mwaka 2015 ili kujiruhusu kugombea tena uchaguzi mwaka uliofuata.

**ESWATINI,** yupo mkali mwingine ambaye ni kiongozi wa ufalme, zamani ukiitwa Swaziland lakini leo amebadilisha jina la taifa linaitwa 'eSwatini' ni Mfalme Mswati III aliyefanya kazi hiyo. Ameingia kwenye jumba la kifalme kuanzia 1986 hadi sasa.

Anatajwa kuwa ni mfalme wa mwisho kabisa wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, Mswati mwenye miaka 51, alitawazwa Aprili 1986 hadi leo.Ni mbabe vyama vya siasa na upinzani vimepigwa marufuku nchini eSwatini, ambayo hapo awali ilijulikana kama Swaziland, kuanzia mwaka 1973, hakuna anayeruhusiwa kuwika mbele ya baba na uongozi ni wa chama kimoja.

**ERITREA**, mambo ni magumu pia huko king'ang'anizi ni Rais Isaias Afwerki, alianza mwaka 1993 hadi sasa akiwa na miaka 74, ameitawala Eritrea tangu ilipopata uhuru wake kutoka kwa Ethiopia.

Hakujawahi kuwa na uchaguzi wa kitaifa nchini Eritrea, ambayo makundi ya haki za binadamu yanachukulia kuwa mojawapo ya mataifa kandamizi zaidi duniani.

**DJIBOUTI** kuna changamoto kama hizo pia, Ismail Omar Guelleh, amekaa ikulu tangu 1999 hadi sasa Guelleh (72), alichaguliwa kumrithi mjomba wake, kiongozi wa uhuru Hassan Gouled Aptidon. Alichaguliwa tena kwa muhula wa nne wa miaka mitano kuanzia 2016.

**MOROCCO** Afrika Kaskazini, hakupoi nako mzee amezoea ikulu ni Mfalme Mohammed VI kuanzia mwaka 1999 hadi sasa Mohammed VI, akiwa na miaka 56, alitawazwa wakati baba yake Hassan II, alipokufa kwa mshtuko wa moyo.

Familia ya kifalme ya Morocco imetawala tangu 1631, na kuifanya kuwa taifa la viongozi wenye nasaba kongwe zaidi duniani .

**UGANDA** Yoweri Museveni amekuwa madarakani kwa miaka 36. Alichukua madaraka Januari 1986 baada ya kushinda vita vilivyomng'oa dikteta katili Idi Amin Dada. Alichaguliwa kwa muhula wa tano Februari 2016.

**RWANDA** yuko Paul Kagame amechukua nchi tangu 2000 hadi leo, akiwa na miaka 62, alionekana na watu wengi kama shujaa mwenye mamlaka halisi nchini Rwanda baada ya kuongoza jeshi la waasi ambalo lilimaliza mauaji ya kimbari ya 1994.

Alichaguliwa rasmi kuwa rais na bunge la kitaifa mwaka wa 2000 na akabadilisha katiba mwaka wa 2015 ili kuongeza ukomo wa muda, hatua ambayo inaweza kumuacha madarakani hadi 2034 na sasa anaendelea kupeta.

**VYAMA VIKONGWE**

Hivi navyo vinapatikana kwa wingi Afrika Kusini ya Jangwa Sahara cha kwanza kwa uzee ni Chama cha African National Congress (ANC) cha Afrika Kusini. Kilianzishwa mwaka 1921 kama chombo kinachotafuta haki za kijamii na kisiasa kwa niaba ya Waafrika Weusi.

ANC ilibeba matarajio ya watu Weusi ambao walitaka kujitawala katika nchi yao na kipindi ambacho kilisisitiza upendeleo kwa walowezi wa Afrika Kusini ambao ni Wazungu.

Namibia kipo chama kikongwe ni SWAPO ni chama cha kisiasa na vuguvugu la zamani la uhuru nchini Namibia. Chama hicho kilichoanzishwa mwaka wa 1960, kimekuwa chama tawala nchini Namibia tangu nchi hiyo ilipopata uhuru mwaka 1990. SWAPO inaendelea kutawaliwa na kuongozwa kwa idadi kubwa na ushawishi wa kabila la wa-Ovambo.

Nchini Botswana kuna BDP kilianzishwa na Sir Seretse Khama, Novemba 1961 na baadaye akawa Rais wa Botswana kimeishi miaka 61 sasa kimeshikilia urais na wingi wa viti vya Bunge tangu uhuru. Wengine hukiita chama cha Khama.

**FRELIMO** ni chama cha siasa cha kisoshalisti cha kidemokrasia nchini Msumbiji. Ni chama kikuu nchini Msumbiji na kimeshinda viti vingi katika Bunge la Jamhuri katika kila uchaguzi tangu uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi nchini humo mwaka 1994. Historia inaeleza kuwa kilianzishwa,Juni 25, 1962 jijini Dar es Salaam na Samora Machel.

Zimbabwe kuna African National Union - Patriotic Front (ZANU-PF) ni chama cha kisiasa ambacho kimekuwa chama tawala cha Zimbabwe tangu uhuru mwaka 1980 ilipopata uhuru hadi leo. Kilianzishwa Desemba 1963 na Robert Mugabe na Joshua Nkomo wote ni marehemu.

**CCM** ni miongoni mwa vyama vikongwe barani Afrika kilizaliwa mwaka 1977 baada ya kuunganisha TANU na AfroShiraz Party ya Zanzibar. Kimeshinda uchaguzi wa urais na wabunge kwa miaka yote tangu TANU ilipoanzishwa mwaka 1954 kwa upande wa Tanzania Bara.

Kadhalika ASP kwa upande wa Zanzibar baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 . Bila shaka kama TANU ingebakia bila kuungana na ASP kuwa CCM, kingekuwa chama kingongwe zaidi Afrika kilichosalia madarakani kikiwa na miaka 66. Kadhalika ASP nalo ingekuwa chama cha pili kwa ukongwe kinachosalia madarakani kingekuwa na miaka 55 baada ya kuanzishwa rasmi Februari 5, 1957.

***MITANDAO***



Mfalme Mswati III

Teodoro Obiang

Isaias Afwerki

**PICHA ZOTE: MTANDAO**





## Matumizi kemikali chanzo cha maradhi PID kwa wanawake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MATUMIZI ya kemikali kujisafishia kwenye sehemu za siri kwa wanawake ni miongoni mwa sababu zinazochangia kushamiri kwa maambukizi katika mfumo wa uzazi wa mwanamke (PID), imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe juzi, mtaalamu wa magonjwa ya wanawake, Dk. Abdul Issa wa Hospitali ya Matovolwa jijini hapo, alisema ndani ya saa 12 kwenye hospitali hiyo hupokea wagonjwa wa PID 10 huku akitaja sababu zinazochangia hali hiyo.

"Njia ya kwanza ya maambukizi ni matumizi ya kemikali kujisafishia katika njia ya uke kwa wanawake, kutumia sabuni zenye manukato kwa wingi kusafisha, pia njia ya uzazi wa mpango ya lupu inasababisha maambukizi kutokana na matumizi ya muda mrefu kuchangia kushusha kinga za uke," alisema.

Alisema, kama mtu anapata maambukizi ya njia ya mkojo kwa muda mrefu (UTI) inachochea kupata PID.

"Pia kuwa na wanaume wengi hiyo ndio sababu kubwa sana kwenye ugonjwa wa PID," alisema.

Alitaja dalili za ugonjwa huo ni kupata miwasho eneo la siri, kuumwa kiuno, maumivu ya tumbo na kutokwa uchafu.

Mtaalamu huyo alisema hali hiyo husababisha baadhi ya wanawake kupata tatizo la ugumba na saratani ya mlango wa kizazi.

"Ukiwahi kupata matibabu unaweza kuondokana na tatizo hili, kwa kuwa si ugonjwa wa kuzaliwa nao," alisema.

Alitoa wito kwa wanawake kuangalia afya zao mara kwa mara ili kujiepusha kupata ugonjwa huo.

# CAG aagizwa ukaguzi maalum Kigoma Ujiji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ameagizwa kufanya ukaguzi maalum kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, kwenye miradi ya ujenzi wa stendi, maji na machinjio.

Agizo hilo kwa CAG limetokana na maelezo yaliyotolewa na viongozi wa halmashauri hiyo kutojitosheleza.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (LAAC), Grace Tendega, alitoa agizo hilo juzi baada ya kukutana na manispaa hiyo kuchambua hoja za ukaguzi zilizoisha Juni 30, 2021.

"Mwaka 2017 halmashauri hiyo ilikuwa na maagizo ya CAG, ambapo walikuwa na mradi mkubwa wa ujenzi wa stendi Sh. milioni 338.5 lakini bahati mbaya maelekezo hayo hayakutekelezwa kwa sababu hakukuwa na vielelezo ambavyo CAG amevipata.

"Ingawa mkurugenzi aliiambia kamati kuwa kuna fedha zimepelekwa benki, hakuna vielelezo kuwa fedha hizo zilipelekwa. Kamati tumeamuru ufanyike ukaguzi maalum kwenye eneo hili la Sh. milioni 338, zirejeshwe kwa kuwa ni fedha za wananchi zilitolewa kwa ajili ya miradi hiyo," alisema.

Tendega, alisema kamati imeagiza pia litekelezwe takwa la kisheria la kutoa fedha asilimia nne kwa wanawake, asilimia nne kwa vijana na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu ambapo wao wanatoa zaidi kwa wanawake.

"Unakuta asilimia nne kwa wanawake inazidi na vijana wao wanapata kidogo na watu wenye ulemavu wanawapa kidogo. Tumewahimiza wakaendeshe mafunzo kwa maofisa maendeleo ya jamii ili wapate sawa maana lile ni takwa la kisheria," alisema.

Alisema, hata kama vijana hawarejeshi wapewe elimu ya fedha na ukopaji wa fedha hizo.

Pia, alisema kamati hiyo imechambua ripoti ya CAG ya Halmashauri ya Kakonko mkoani Kigoma na kubaini kuwa ina makusanyo yasiyofika Sh. bilioni moja, hivyo kusababisha kuchechemea kimaendeleo.

"Kuna wakati waziri alisema halmashauri ambazo hazitafikisha Sh. bilioni moja zitafutwa. Tumewaambia waangalie vyanzo vya mapato kwa sababu wako mpakani lakini wana vyanzo vingine vya mapato wakiamua kuwekeza kwenye kilimo wanaweza kupata fedha. Lakini waangalie maeneo muhimu ambayo tunaweza kupata fedha," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema, kamati imeagiza vyanzo vya mapato vipya viangaliwe kwa kuwa bila hivyo halmashauri itashindwa kujiendesha.

"Pia wana hoja nyingi za CAG lakini wanajibu bila viambatanisho. Kama hakuna kiambatanisho hiyo hoja haiwezi kufungwa, itafungwa kama kuna viambatanisho," alisema.



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mbegu za Kilimo nchini (ASA), Dk. Sophia Kashenge (kulia), akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi wa Kampuni ya Pro Agro Global Ltd, Bryson Maro, jijini Dodoma jana, baada ya kutiliana saini mkataba wenye thamani ya Sh. bilioni 18, kwa ajili ya utekelezaji wa kilimo cha umwagiliaji kwenye mashamba ya Msimba, Ngaramtoni na Kilimi katika mikoa ya Morogoro, Arusha na Tabora. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# STAMICO yapunguza utegemezi kwa serikali

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIRIKA la Madini la Taifa (STAMICO), limepunguza utegemezi wa fedha za serikali kutoka asilimia 89 mwaka 2018/19 hadi asilimia 9.2 mwaka 2022/23.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Madini, Augustine Ollal, aliyesema hayo jana alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwenye kikao kilichofanyika bungeni jijini Dodoma.

Ollal, alisema STAMICO imeanzisha miradi yake kutokana na fursa mbalimbali zinazojitokeza ili kuongeza vyanzo vya mapato ya ndani na kupunguza utegemezi serikalini ili shirika lijiendeshe kibiashara.

"Mapato ya shirika yameongezeka kutoka Sh. bilioni 5.86 kwa mwaka wa fedha 2019/20, Sh. bilioni 19.6 kwa mwaka wa fedha 2020/21 na Sh. bilioni 48.5 kwa mwaka wa fedha 2012/22,"alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Vanance Mwasse, alisema baada ya kero ya kupanda kwa bei ya nishati ya mafuta, shirika limeangalia namna bora ya kulipa deni lake na kwamba mpaka sasa shirika limelipa zaidi ya Sh. bilioni 1.7 na linategemea kuanza kulipa Sh. milioni 600 kila mwezi mpaka deni litakapomalizika.

Naye Mbunge wa Nyasa, Stella Manyanya, alisema serikali iangalie namna ya kulisaidia shirika kulipa mkopo wa Sh. bilioni 18.75 ili wadai mbalimbali wapate haki zao na kufanya biashara baada ya kulidai shirika hilo kwa muda mrefu.

Mbunge wa Ulanga, Salim Hashim, aliitaka serikali kuangalia namna ya kuziongezea halmashauri mapato yatokanayo na sekta ya madini. Alisema tozo zitokanazo na mrabaha ambayo ni asilimia saba ipunguzwe kwa asilimia mbili ili asilimia tano iende serikali kuu na asilimia mbili ibaki kwenye halmashauri husika.

Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, aliishukuru kamati hiyo kwa maagizo iliyoyatoa na kuahidi kuyafanyia kazi maagizo hayo yenye lengo la kuiboresha sekta ya madini.

"Wizara ya Madini tutaendelea kufanyia kazi maelekezo na ushauri wa Kamati ili kuhakikisha sekta ya madini inakuwa na hatimaye kufikia mchango wa asilimia 10 kwenye pato la taifa ifikapo mwaka 2025," alisema.





# Wadau wa pareto walia na 'vishoka' kuwaibia wakulima

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa pareto, wameiomba serikali mkoani Mbeya, kusaidia kuchunguza na kuwakamata watu wote wanaofadhili ununuzi wa zao hilo nje ya utaratibu 'vishoka' kwa madai kuwa wanawaibia wakulima na kudhoofisha jitihada za kuendeleza zao hilo.

Ombi hilo limetolewa juzi na wadau hao wakati wakikabidhi msaada wenye thamani ya Sh. milioni 40, ikiwa ni vifaa vya elimu kwa wanafunzi zaidi ya 600 wa shule za msingi, na mablanketi kwa ajili ya wazee 400 wanaolima pareto katika Kata ya Santilia, wilayani Mbeya.

Mwakilishi wa Kampuni ya Pareto Tanzania (PCT), Jamal Issa, alisema wakulima wanakabiliwa na tatizo kubwa la vishoka kutoka kwa wanunuzi ambao hununua zao hilo kwa bei ndogo.

Alisema, hali hiyo inawaumiza kwa kuwa hawapati faida licha ya kutumia nguvu kubwa ya kuzalisha.

Alisema mara kadhaa wanazungumza na viongozi wa kata na halmashauri kuhusu vishoka hao, lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa kuwadhibiti.

"Ni muda sasa wakulima hao kuangaliwa kwa jicho la huruma ili waweze kupata faida kutokana na kilimo chao cha zao la pareto ambalo kwa Mkoa wa Mbeya ndiyo inaongoza kwa uzalishaji na ubora nchini," alisema Issa.

Akizungumzia suala la vishoka hao kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, Ofisa Tarafa wa Isangati, Aron Sote, alisema tayari hatua zimeanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wakulima kuacha kuwauzia vishoka mazao yao.

Alisema, kazi kubwa wanayoifanya ni kuwahamasisha wakulima hao kujiunga kwenye vyama vya ushirika ili kuuza mazao yao kwa pamoja na kupanga bei itakayowanufaisha.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Diwani wa Kata ya Santilia, Mwajuse Mwarwanda, alisema tatizo kubwa linalowakabili wakulima wa eneo hilo ni soko la uhakika.



Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Absa Tanzania, Aron Luhanga (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi kwa mara ya kwanza nchini wa huduma ya kutoa fedha katika mashine ya ATM bila ya kuwa na kadi halisi mfumo wa (QR Code). Wengine kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Miradi, Irene Mushi, Mkuu wa Kitengo cha Digitali na Ubora wa Huduma kwa Wateja, Samuel Mkuyuna (wa pili kulia) na Meneja Huduma za Kidigitali, Adam Emmanuel. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Polisi yatangaza operesheni kamata bodaboda

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani hapo, limetangaza operesheni ya kuwakamata madereva wa bodaboda wakataokuvunja sheria za usalama barabarani ikiwamo kupita kwenye taa za kuongoza magari bila kufuata utaratibu.

Mkuu wa Operesheni wa Jeshi la Mkoa wa Mbeya, Abdi Issango, alitoa kauli hiyo jana kwa niaba ya Kamanda wa Jeshi la Polisi, Ulrich Matei, wakati akitoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva hao.

Alisema, operesheni hiyo itahusisha barabara zote za Mkoa wa Mbeya na dereva yeyote wa bodaboda atakayebainika amezidisha abiria zaidi ya mmoja, hajaheshimu taa za kuongoza magari, atakamatwa na kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

"Tutafanya operesheni kubwa ili madereva wote wasiotii sheria wakamatwe na kuadhibiwa kila anayefanya biashara ya bodaboda azingatie kanuni za usalama barabarani, waache kupakia abiria zaidi ya mmoja (mishkaki), wavae kofia ngumu, lakini pia wawe mabalozi wazuri wa kuripoti vitendo vya kiuhalifu," alisema ACP Issango.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Yusuph Kamota, aliwataka madereva hao kujiunga kwenye vikundi kwa ajili ya kuimarisha ulinzi shirikishi.

Alisema, vikundi hivyo kupitia umoja wa madereva bodaboda vitasaidia kukabiliana na vitendo vya uhalifu kupitia uongozi wao ambao utakuwa na jukumu ya kuzuia ubakaji, wizi na mauaji.

"Hakikisheni bodaboda hamjihusishi na vitendo vya uhalifu wa aina yoyote iwe ni kwa kubeba mali za wizi au kusafirisha wahalifu na badala yake amewataka kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu ili wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria," alisema Kamotta.

Mwenyekiti wa Chama cha Madereva bodaboda Jiji la Mbeya, Aliko Fwanda, amelihakikishia Jeshi la Polisi kuzingatia sheria zote za usalama barabarani.

# Zaidi ya wateja 700 wafungiwa mita za LUMAKU

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JUMLA ya wateja 713, wameunganishiwa mita za Malipo ya Kabla (LUMAKU), kupitia huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini hapo ikiwa ni mpango mkakati wa mamlaka hiyo na serikali kupitia Wizara ya Maji ya kuagiza wananchi wafungiwe mita hizo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya, CPA Gilbert Kayange, mamlaka hiyo ilianza kufunga mita hizo mwaka 2015, kwa kuwafungia wateja 50 kama majaribio ya ufanisi na baada ya kubaini utumiaji wake kuwa mzuri ilifanya mchakato wa kuagiza mita nyingine zenye ubora zaidi unaokidhi kwa mazingira ya jiji hilo.

Alisema, licha ya mita hizo kuwa na gharama kubwa ikilinganishwa na mita za malipo ya baada, mamlaka imeanza kufanya mita hizo kimkakati kwa kuwafungia wateja wa taasisi, biashara na baadhi ya wateja wa majumbani.

"Katika kuboresha huduma hiyo na kuhakikisha inawafikia wananchi mamlaka yetu mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kununua mita za LUMAKU 1,000 na zitawafikiwa wateja wote," alisema Kayange.

Kuhusu wimbi la vishoka mitaani CPA, Kayange alisema ni miongoni mwa vikwazo vinavyoikabili mamlaka hiyo kwa sababu wanachangia kwa kiasi kikubwa maunganisho ya maji yasiyokuwa halali kitendo kinachoinyima serikali mapato huku wengine wakikosa huduma ya maji kikamilifu.

Alisema katika kupambana na mafundi vishoka, mamlaka hiyo, inashirikiana na wadau mbalimbali vikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi wa serikali wa eneo husika na wasamaria wema kupata taarifa za wizi wa maji.

Alibainisha mwaka 2020/2021 jumla ya watuhumiwa 23 walikamatwa kwa kosa la kuwaunganishia wateja huduma ya maji kinyemela na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria na wanaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali huku wakitoa dau la Sh. 200,000 kwa yeyote atakayefanikisha kutoa taarifa za uwapo wa vishoka.

Hata hivyo, Kayange aliwahakikishia wakazi wa Mbeya kuendelea kupata huduma ya majisafi na salama kwa wakati bila upendeleo na kutoa taarifa linapojitokeza tatizo.

Hivi karibuni baadhi ya wananchi walitoa malalamiko kwa mamlaka hiyo kutoa huduma za maji kwa upendeleo ukiwamo utaratibu wa kujiunga na huduma hiyo waliyodai inatolewa kipaumbele kwa mtu wanayemfahamu.

Kayange, alisema mamlaka hiyo inafuata utaratibu kwa wateja waliokamilisha mahitaji yote ya maunganisho ya huduma mapema na kutaja maeneo yanayopata maji kwa mgawo kuwa ni Uyole, Isyesye, Ituha, Shewa na baadhi ya maeneo ya Sae.



## Wawekezaji waaswa kufuata masharti kuepuka matapeli

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wawekezaji wenye nia ya kuwekeza nchini kufuata maelekezo na masharti ya uwekezaji ili kuepuka utapeli unaojitokeza.

Aliyasema hayo juzi Ikulu Zanzibar wakati akijibu maswali katika kikao chake na waandishi wa habari, utaratibu aliojiwekea kila mwisho wa mwezi kuzungumza nao. Alisema sheria za uwekezaji zipo wazi na mwekezaji mwenye nia ya kuwekeza anatakiwa kwenda Mamlaka Huru ya Vitega Uchumi na Uwekezaji (ZIPA) na kupata mwongozo na masharti ya kuwekeza.

Dk. Mwinyi alitoa ufafanuzi huo baada ya kuulizwa kuhusu mwekezaji mmoja ambaye alikuja nchini na kuonesha nia ya kuwekeza, lakini inadaiwa alitapeliwa eneo la ardhi na kufungua kesi mahakamani ambayo imekuwa ikisuasua.

"Jamani hata nyinyi waandishi wa habari hebu waelimisheni wawekezaji wetu...tunao utaratibu unaofahamika kwa mujibu wa sheria ambapo Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi (ZIPA) ndiyo inayohusika na mambo hayo lengo ni kuondosha urasimu uliokuwapo awali," alisema.

Alizitaka manispaa na mabaraza ya mji kujipanga vizuri kuhakikisha zinatekeleza majukumu yake ya kutoa huduma za usafi kwa wananchi ikiwamo uzoaji wa taka.

Alisema hatosita kuwawajibisha watendaji wa manispaa hizo ambao watashindwa kutekeleza majukumu yoa kwa sababu hivi sasa manispaa zimepunguziwa majukumu yao na kazi yao kubwa ni kuweka usafi wa mji.

Kadhalika, alisema hajaridhishwa na usafi wa mji katika manispaa kwa sababu barabra kuu anayopita yeye mara kwa mara ndiyo inayonekana inasafishwa, huku maeneo mengine hali ikiwa mbaya.

Aliwataka watendaji wa mabaraza hayo kujipanga vizuri kuhusu usafi wa mji na kama watashindwa kujirekebisha atafanya mabadiliko ya kuteua viongozi wengine wa mabaraza hayo.

# Mwinyi: Serikali imeanza mchakato kuimarisha maslahi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali imeanza mchakato wa kuimarisha maslahi ya watendaji katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili kulinda nguvu kazi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar, alipozungumza na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Tanzania (CAG), Charles Kichere.

Alisema serikali inatambua umuhimu wa kazi inayofanywa na watumishi hao (wakaguzi) na tayari mchakato wa kuimarisha maslahi yao umeanza kuambatana na mfumo uliopo wa makundi, akitolea mfano wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA), inayopaswa kuwa katika kundi la taasisi zinazozalisha kama Bandari.

Alisema kuna umuhimu wa kuondoa tatizo la kimaslahi kwa watendaji wa taasisi hiyo kwa kuzingatia kuwa wengi wanaokaguliwa wana maslahi makubwa na kuwapo uwezekano wa kuondoka na kwenda kutafuta maslahi makubwa maeneo mengine.

Akigusia ukaguzi wa vyombo vya Muungano vilivyoko Zanzibar, Dk. Mwinyi alisema anafarijika kuwapo kwa ushirikiano wa taasisi mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Tanzania na ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, huku akibainisha kuwapo changamoto kubwa katika vyombo hivyo kutokaguliwa.

Alisema kuna tatizo kubwa katika Idara ya Uhamiaji Zanzibar, "kuna wakati ilitumwa kamati kwenda kufanya ukaguzi na kugundua kiasi cha shilingi bilioni nane kilikuwa kimepotea ndani ya miezi sita, bado kuna kazi ya kufanya".

Alisema kuna uwezekano wa vyombo hivyo vya Muungano vinavyofanya kazi Zanzibar kujificha nyuma na kutokuwapo katika ukaguzi, jambo alilosema linapaswa kurekebishwa, akibainisha hatua ya taasisi hizo kufanya kazi kwa pamoja kutasaidia juhudi hizo.

Alipongeza hatua ya kuondoka kwenye ukaguzi wa vitabu na kwenda kwenye miradi ili kuona uhalisia.

Alisema Zanzibar inaelekea kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia na kwamba kuna mambo mengi ya kujifunza kutoka Tanzania Bara ambayo tayari imepiga hatua katika sekta hiyo, sambamba na kuwapo umuhimu wa kuwajengea uwezo watendaji (wakaguzi).

Naye CAG Kichere, alimpongeza Dk. Mwinyi kwa kazi kubwa na maono yake katika kuiletea Zanzibar maendeleo pamoja na kusimamia rasilimali za nchi.

Alisema Taasisi CAG Tanzania pamoja na ya CAG Zanzibar zimekuwa na mashirikiano mazuri, baadhi ya nyakati huunganisha nguvu katika utekelezaji wa majukumu hususan katika miradi mikubwa pamoja kujengeana uwezo.

Alisema taasisi hizo kama zilivyo sawa katika utekelezaji wa majukumu yake, zinakabiliwa na changamoto zinazolingana, ikiwamo ile ya maslahi, hivyo akaziomba serikali zote mbili kuangalia uwezekano wa kuondokana na changamoto hiyo.

Kwa upande wake, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, Dk. Othman Abassa, alisema kumekuwapo ushirikiano mkubwa kati ya taasisi hizo mbili, akitolea mfano wa hatua za hivi karibuni, Ofisi ya CAG Tanzania kuisaidia CAG Zanzibar kufanikisha ukaguzi katika taasisi za Muungano, ikiwamo BoT, TRA na Ofisi za Mabalozi , ilipokuwa ikiendesha ukaguzi kwa kuwawezesha watendaji wake kufika hadi mikoa ya Tanzania Bara na kuwasomesha kwa gharama za Ofisi ya CAG Tanzania Bara.

Alisema katika kipindi kifupi kijacho, taasisi hizo zinatarajiwa kukamilisha mchakato wa utiaji saini hati za ushirikiano (MOU).



Waziri wa Maendeleo ya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe, akiwajulia hali watoto waliolazwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, jijini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yaridhia fao la kujitoa wanachama ZSSF

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema Serikali ya Zanzibar imeridhia kuanza kutoa fao la kujitoa kwa hiari kwa wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) ili kufaidika na fedha walizochangia.

Aliyasema hayo jana mjini hapo wakati akifungua mkutano wa mifuko ya hifadhi ya jamii kwa nchi za Afrika ya Mashariki (ECASSA).

Alisema serikali imefikia uamuzi huo baada ya kubainika watu wengi wakiathirika na mfuko huo baada ya kupoteza ajira katika kipindi cha mlipuko wa maradhi ya UVIKO - 19 na wafanyakazi wengi katika sekta binafsi kuacha kazi.

Alisema kitendo cha wafanyakazi wengi kupoteza ajira katika sekta binafsi ikiwamo ya hoteli za kitalii kumesababisha ugumu wa maisha kutokana na fedha walizoziweka kushindwa kuzipata.

Kadhalika, waziri alifafanua kuwa marekebisho hayo kwa kiasi kikubwa yataongeza ari ya wanachama wanaoweka fedha katika mfuko huo hasa katika sekta binafsi ambayo imekuwa ikiongezeka kwa kiwango kikubwa. Alisema marekebisho hayo ni muhimu yanayokwenda na wakati wa uwekezaji katika sekta binafsi ambayo yataongeza ari kwa wafanyakazi na uwekezaji wake.

Naye Mkurugenzi wa ZSSF, Nassor Shaali Ameir, alisema suala la kutokuwapo kwa fao la kujitoa ni moja ya changamoto kubwa iliyokuwa ikiwakabili wanachama wake ikiwamo waliopoteza ajira.

Alisema wanachama wengi waliathirika na kupoteza ajira katika kipindi hicho ambapo mfuko ulipata usumbufu mkubwa kutoka kwa wanachama wake kudai mafao wakati sheria inayowataka kupata haki hiyo haipo.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema mifuko ya hifadhi ya jamii imekuwa sehemu ya maisha ya wafanyakazi pamoja na kuchochea maendeleo ya taifa.

Alisema mifuko hiyo inahitaji kwenda na mabadiliko ya wakati ikiwamo kuwahudumia wanachama wake katika kumudu gharama za maisha na kuwa nafuu zaidi.


**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 123 OF 2022**
**In the matter of the estate of the late of the late RECHARD PETRO TOROKAA Of Maendeleo street, Chamwino District within Dodoma Region.**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration by PETER RICHARD TOROKAA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**


**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **26 Day of 9,2022.**
**Dated at Dodoma this 5TH day of September, 2022.**



**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA.**
**MAHALI MASWA.**
**MAOMBI MAKUBWA NA.21 YA MWAKA 2022**
**KATI YA**
**JESCA LIMI MGEJA..............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1.KWILASA KULABA**
**2.GIGWA SALUMU**
**3.DAUD JOHN**
**4.PASCHAL JOHN**
**5.MBUKE JOSEPH**
**6.JAMES JOHN ............WAJIBU MAOMBI**

**WITO/TAARIFA**


**Kwa: DAUD JOHN POPOTE ALIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Maombi dhidi yenu katika Baraza hili la wilaya ya Maswa.Maelezo ya madai yanaweza kupatika hapa Barazani.Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi(WSD)kabla ya tarehe 26.09.2022.
Pia unajulishwa kuwa Maombi haya yamepangwa kutajwa siku ya tarehe 26.09.2022 saa 2;30 asubuhi mbele ya Mhe.J.T.Kaare Mwenyekiti,Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya-Maswa.
Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakadi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa,Baraza litalazimika kusikiliza Maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.
IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 30.08.2022




**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 115 OF 2022**
**In the matter of the estate of the late of the late COSMAS MNUBI within Dodoma City.**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration by GEOFREY COSMAS MNUBI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **19 Day of 9,2022.**
**Dated at Dodoma this 9 day of 8, 2022.**



## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KAHAMA OIL MILLS** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.258 AFR** aina ya **TALLER.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya jeshi la polisi **KAH/RB/615/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CLEUS KATO Nyasubi** mjini Kahama,anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.721 BZN** aina ya **TELLA.**
Yeyote atakayeiona ataoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya jeshi la polisi. **KAH/614/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LILIAN .E. MAPUNDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0836/0082/15** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KILUVYA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2015.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA : KIL/MOS/RB/516905/2019**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 116 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JULIANA SEVERINI NYENZA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**MOSSES DEOGRATIAS MSILA............... 1st PETITIONER**
**AND**
**BAHATI SEVERINI NYENZA ............... 2nd PETITIONER**
**FORM 58**
**APPLICATION FOR APPOINTMENT OF ADMINISTRATOR OF SMALL ESTATE**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 27th Day of September, 2022.
**Dated at DODOMA this 06st day of September 2022**



**RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SEVERINE JONAS MHUMPHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye No. **S2327-0169** kilichotolewa na baraza la mtihani kupitia AZIMIO SECONDARY SCHOOL mwaka 2014. yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/350126/2022.**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**




**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wahimizwa kudhibiti ubora usalama bidhaa

**Na Joseph Mwendapole**

MAOFISA afya na biashara wa halmashauri zote za mkoa wa Mwanza, wametakiwa kuweka kipaumbele udhibiti wa ubora na usalama wa chakula na vipodozi.

Agizo hilo lilitolewa jana na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Daniel Machunda, wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa maofisa afya na biashara wa halmashauri za Mwanza.

Mafunzo hayo yalihusu kujengewa uelewa kuhusu sheria, kanuni na miongozo inayohusika na utekelezaji wa majukumu ya ushirikiano baina ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mafunzo hayo yaliyoendeshwa na TBS yalifanyika katika Ukumbi wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), Buzuruga, jijini Mwanza na ni ya awali na watumishi waliolengwa ni maofisa kutoka katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa, halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji.

Alisema azma ya serikali ni kuhakikisha inakuwa na mtandao mkubwa unaoshughulikia masuala ya udhibiti wa ubora na usalama wa chakula na vipodozi kote nchini.

"Kwa kulitekeleza hili serikali imeamua kuwatumia wakaguzi walio chini ya ofisi ya TAMISEMI katika shughuli za udhibiti wa bidhaa husika ili kulinda afya za watumiaji katika maeneo yao," alisema.

"Kwa kufanya hivi itasaidia kuhakikisha shughuli za udhibiti zinafanyika kwa haraka na ufanisi zaidi," aliongeza.

Pia aliwataka washiriki wafahamu kuwa sheria, kanuni na mwongozo tajwa zimepitia mchakato wote unaotakiwa na zimepata baraka kutoka ofisi ya TAMISEMI na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

"Hivyo watumishi wana wajibu wa kuelewa na kutekeleza makubaliano yaliyoainishwa kwenye sheria, kanuni na miongozo husika ninaamini kuwa mafunzo haya ni njia mwafaka ya kuleta tija zaidi katika juhudi za kuleta maendeleo katika udhibiti wa bidhaa za chakula na vipodozi katika mkoa huu," alisema

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora wa TBS, Lazaro Msasalaga, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo watumishi na kuongeza ufanisi wa kazi.

Alisema mafunzo hayo tayari yamefanyika kwenye halmashauri za mikoa ya Mtwara, Tanga, Pwani na Kigoma na yanatarajiwa kufanyika mikoa yote nchini yakilenga watumishi kutoka idara za afya na biashara kutoka TAMISEMI.

"Lengo kuu la mafunzo haya ni kuwapa walengwa elimu kuhusu sheria, kanuni na miongozo inayohusika na utekelezaji wa majukumu ya ushirikiano baina ya TBS na TAMISEMI,"alisema.

Alisema TBS imekuwa ikifanya shughuli za ukaguzi na udhibiti kwa kushirikiana na watumishi kutoka katika ofisi za Halmashauri, hivyo anaamini mafunzo hayo yataongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa.

# Watoto 306 wapoteza maisha kwa kupakwa kinyesi kitovuni

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WATOTO 306 katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, wamepoteza maisha kutokana na wazazi wao kuwapaka poda na kinyesi cha wanyama katika vitovu ili vikauke na kupona haraka.

Watoto hao wamefariki dunia katika kipindi cha mwaka jana kuanzia Januari hadi Desemba huku vifo vya wajawazito vikiwa tisa kati ya hivyo vinne vilitokea manispaa hiyo na vitano vikitokea sehemu mbalimbali ikiwemo Uyuwi- Tabora, Mwakata, Lunguya na Mwanase- Msalala kwa sababu wanakwenda kutibiwa hapo.

Mratibu wa Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto katika Wilaya ya Kahama, Caroline Marcel, aliyabainisha hayo juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake wanavyopambana kuhakikisha vifo vya watoto wachanga na wajawazito vinatokomea kwa kutoa elimu.

Alisema wazazi wamebuni mbinu mpya ya kutibu vitovu vya watoto wao wachanga kwa kuweka poda na kinyesi cha wanyama ili kikauke na kupona haraka hali ambayo ni hatari kiafya kwa watoto.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, hali hiyo imekuwa ikisababisha kupoteza maisha na wanaendelea kutoa elimu ya afya ya uzazi kupambana na jambo hilo.

Alisema sababu nyingine ni wazazi wao kuchelewa kuanza kliniki, kuzaliwa kabla ya siku (njiti), kupata homa kali na kufa, kutumia dawa za kungeza uchungu wakati wa kujifungua hali ambayo inasababisha kupasuka kizazi na mtoto kunywa maji machafu tumboni.

Marcel alisema kati ya vifo hivyo, watoto 48 walifariki dunia ndani ya siku saba baada ya kuzaliwa, 128 walizaliwa wakiwa wameshakufa na 130 wamezaliwa wakiwa wamefia tumboni zaidi ya siku mbili na wazazi wao wangewahi kuanza klikini baada ya kuhisi ni wajawazito vifo hivyo visingetokea.

"Kuna wajawazito wanahudhuria kliniki ipasavyo lakini wanapoteza maisha kwa kupata kifafa cha mimba na wengine mtoto anajinyonga awapo tumboni kadiri anavyozidi kusogea au kugeuka," alisema.

Alisema watoto wanaozaliwa na ulemavu hutokana na wazazi kuchelewa kuanza huduma ya kliniki, hivyo kuwa na watoto wenye utumbo wazi, mgongo wazi, kichwa wazi, na ili kuondoa hayo wamekuwa wakitoa elimu ya uzazi salama kipindi cha kliniki.

Naye Agnes Joseph, mkazi wa Nyashimbi, alisema awali alikuwa akipata ujauzito na kujifungulia nyumbani kwake ilikuwa fahari na kuonekana ni jasiri na sasa ana watoto watano kati ya hao wawili amejifungulia kituo cha afya baada ya kupata elimu ya afya ya uzazi.

Alisema,jirani yake aliwahi kujifungua mtoto mwenye tumbo wazi na alichukua muda wa siku mbili na kupoteza maisha. Alipofuatiliwa kwa nini hali hiyo imetokea, alipata elimu na sasa hawezi kuzalia nyumbani wala kwa waganga wa jadi.




Diwani Kata ya Mabwepande, Muhajirina Obama (katikati), akipanda mti kuzindua kampeni rasmi ya upandaji miti inayoendeshwa na Taasisi ya Mother of Mercy katika eneo la Mto Mpiji Mabwepande, mkoani Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Gration Mbelwa na Ofisa Mazingira wa Manispaa ya Kinondoni, Hawa Hanti. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Msamaha wa Samia pango ardhi wapaisha makusanyo ya wizara

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amesema mabadiliko ya sera na msamaha wa riba ya pango la ardhi uliotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, yamepaisha makusanyo ya wizara kwa asilimia 56 ndani ya miezi sita.

Kikwete aliyasema hayo jana baada ya kukutana na Kamati ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Utalii kueleza yaliyofanyika katika kipindi cha miezi sita.

"Katika kikao hicho tumeelezea juu ya mambo yaliyokwisha kufanyika na yanayoendelea kufanyika, pia kutoa taarifa ya hali ya makusanyo ambapo katika mwaka wa fedha uliopita makusanyo ndani ya wizara hayakuwa mazuri sana, lakini katika kipindi hiki cha miezi sita ya kwanza tumefikia asilimia 56 ya makusanyo," alisema.

"Mabadiliko ya sera ikiwamo msamaha mkubwa ambao Rais Samia Suluhu Hassan aliutoa kwa wananchi hasa katika malimbikizo ya riba katika makusanyo ambayo yalisababisha watu wengi kushindwa kukusanya hivyo makusanyo yakawa madogo."

Awali, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Ally Makoa, aliagiza Tume ya Mipango ya Ardhi iongeze kasi zaidi ya kupima maeneo yote katika wilaya zote ili kupunguza na kuondoa migogoro.

"Tume imechukua ushauri wa kamati na kila baada ya kipindi tutakuwa tunafuatilia utekelezaji ili tuone ni namna gani Tume imeweza kusaidia taifa letu kuondokana na migogoro ya ardhi ambayo imetapakaa maeneo mengi," alisema.

Pia alipongeza watu wa Chuo cha Ardhi cha Tabora kwa kufanya kazi nzuri ya kuzalisha vijana watakaosaidia katika mipango ya ardhi.

"Tumeshauri chuo kuwajenga vijana katika maadili, wajumbe walizungumzia masuala ya migogoro ambayo yanaanzishwa na watendaji na tumeshauri chuo kuandaa kozi fupifupi kuwakumbusha maadili maofisa wa ardhi ili kujitahidi kusaidia nchi yetu kuepukana na migogoro," alisema.

# NMB JOGGING MGUU SAWA KUELEKEA NMB MARATHON

**Mwandishi Wetu**

WAKATI mbio za NMB Marathon zikitarajiwa kutimua vumbi Septemba 24, mwaka huu, Klabu ya NMB Jogging jana, Jumatatu ilianza kujifua mapema kwa ajili ya kujiweka tayari kushiriki mbio hizo.

Klabu hiyo ya Jogging, ilianza kujiandaa na mbio hizo kwa kushirikiana na klabu mbalimbali ikiwamo EFM Jogging, ambapo walianza maandalizi hayo kwa kukimbia mbio za kilomita nane ambazo ziliaanzia Ofisi za NMB, Posta jijini Dar es Salaam.

Mbio hizo za NMB Marathon, ambazo huu ni msimu wake wa pili kufanyika, zinatarajiwa kurindima katika viwanja vya Leaders, Dar es Salaam ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Meneja wa NMB Jogging, Stella Moto, akizungumzia mbio hizo zenye kaulimbiu ya 'Mwendo wa Upendo' jana, alisema zinafanyika maalum kwa lengo la kuchangisha fedha kwa ajili ya kupambana na matatizo ya fistula kwa kinamama.

Alisema: "Tuna siku chache kabla ya kufika Septemba 24 siku ambayo ndiyo NMB Marathon itafanyika, hivyo tumeona tupashe misuli ili tuwe sawa na kuwakumbusha wadau wetu kuelekea siku hiyo.

"Kama unavyojua lengo kuu la mbio hizi ni kukusanya fedha kwa ajili ya kina mama wenye matatizo ya fistula. Tunawaomba Watanzania mbalimbali kuanzia mmoja mmoja au vikundi tuweze kuungana pamoja kwa ajili ya jambo hili," alisema Moto.

Kwa upande wa mwakilishi wa EFM, Tunu Hassan, alisema: "Hii si mara ya kwanza kwa NMB kurudisha kwa jamii, hivyo nasi tumeona tuungane nao kwa ajili ya jambo hilo.

"Tunawaomba wadau wa michezo na wasio wanamichezo kujitokeza lengo la kuchangia fedha kwa ajili ya kinamama hao, lakini wajitokeze kwa ajili ya kushiriki mbio hizi."




Wanachama wa klabu za kukimbia za NMB na EFM wakiwa katika mazoezi ya pamoja jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni maandalizi ya mbio za hisani za NMB Marathon zenye kaulimbiu ya 'Mwendo wa Upendo' zitakazofanyika Septemba 24, mwaka huu, katika viwanja vya Leaders Club. **MPIGAPICHA WETU**

# Mzunguko wa kwanza Ligi Zanzibar wazaa mabao 15

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MZUNGUKO wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar umemalizika kwa timu zote 16 zinazoshiriki ligi hiyo kushuka dimbani huku jumla ya mabao 15 yakizamishwa kambani.

Kati ya mabao hayo moja tu ndilo lililopatikana kwa mkwaju wa penalti, wakati JKU ikishinda 3-0 dhidi ya Uhamiaji.

Katika mzunguko huo wa kwanza timu zilizofanikiwa kuvuna pointi zote tatu ni KMKM, JKU, Dulla Boys, Malindi, Mlandege na Kipanga, wakati zilizoambulia alama moja kwa kutoka sare michezo yao ni KVZ, Mafunzo, Taifa Jang'ombe na Jamhuri.

Kwa upande wa timu ambazo zimeanza ligi hiyo kwa kuangukia pua ni Kundemba, Black Sailor, Uhamiaji, Chipukizi, Polisi na Zimamoto.

Hadi mzunguko huu wa kwanza unakamilika KMKM, ndiyo iliyofanikiwa kuwa kinara kutokana na kupachika mabao manne ikifuatiwa na JKU yenye matatu, Malindi wakitupia mawili wakati Mlandege na kipanga zikiwa na bao moja moja. Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Hashim Salum, alisema klabu zote zimeelewa vema kanuni katika mzunguko huu ikilinganishwa na uliopita.

Alisema, katika mzunguko huu hakukuwa na changamoto kubwa na kwamba changamoto zilizojitokeza ni za kawaida ambazo hazikuathiri shughuli za uendeshaji wa michezo hiyo.

Salum, alisema Bodi ya Ligi Zanzibar, inamalizia kupitia ripoti zote za mzunguko huu na baada ya hapo itatoa taarifa kwa vyombo vya habari kabla ya kuanza mzunguko wa pili.

Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa pili itaendelea Jumapili wiki hii ambapo michezo ya saa 10 alasiri itakuwa Chipukizi dhidi ya Maafande wa Polisi utakaopigwa Uwanja wa Finya Kisiwani Pemba, Uhamiaji watavaana na Jamhuri Uwanja wa Amaan na Dulla Boys ikiwa dimbani dhidi ya Taifa Jang'ombe katika uwanja huo saa moja usiku.

## Simba Queens kuongeza wa3 CAF

**Na Saada Akida**

KUELEKEA Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, Kocha Mkuu wa Simba, Sebastian Nkoma, amesema ataongeza nyota watatu katika usajili akiwamo kipa wa kigeni.

Simba ambao ni mabingwa wa CECAFA, watauwakilisha ukanda huu katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Oktoba mwaka huu nchini Morocco.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nkoma, alisema kuelekea michuano hiyo mikubwa, anahitaji kujiimarisha zaidi katika madhaifu aliyoyaona kwenye Fainali za CECAFA.

Alisema, mapungufu aliyoyaona ambayo anataka kuyaboresha ni kuongeza kipa, beki mkabaji na mshambuliaji wote kutoka nje kwa ajili ya michuano hiyo pia ligi za ndani.

"Tunaenda kucheza michuano ya kimataifa na Simba inabeba dhamana ya huu Ukanda wa CECAFA, lazima tujiimarishe kuongeza watu bora ili kuungana na walikuwapo kikosini kwa ajili kufikia malengo yetu," alisema Nkoma.

## Rotary Oysterbay yaja na Tamasha la mbio za Mbuzi

**Na Mary Geofrey**

KLABU ya Rotary Oysterbay imeandaa Tamasha la Mbio za Mbuzi zitakazofanyika Novemba 5, mwaka huu kwa lengo la kukusanya fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo sekta ya elimu kuanzia ngazi ya msingi hadi chuo kikuu.

Rais wa Rotary, Krutin Shah, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema katika tamasha hilo wanatarajia kukusanya Sh. milioni 100 kwa ajili ya kusaidia jamii katika upande huo wa elimu.

Alisema, tamasha hilo linafanyika kwa mara ya tatu tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018 kwa kuzingatia maeneo muhimu sita yaliyopewa kipaumbele na Rotary Oysterbay.

Alisema kupitia tamasha hilo, washiriki ambao ni watu wazima na watoto watapata burudani mbalimbali kupitia michezo iliyoandaliwa.

"Mashindano ya mwaka huu yaliyopewa kaulimbiu inayosema, 'Sherehekea tamaduni mbalimbali duniani', yatawavutia mashabiki wapya pamoja na washiriki," alisema Shah.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GAVI AWINDWA BAYERN
MABINGWA wa Ujerumani, Bayern Munich wameingia katika mbio za kumuwania nyota wa Barcelona, Gavi, huku Manchester United na Liverpool zikiaminika tayari zimeanza kumfuatilia kiungo huyo wa Hispania mwenye miaka 18. ***(Bild, via Mail)***

### NAPOLI YAMKANA RONALDO
NAPOLI imekanusha kufanya mazungumzo na mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 msimu huu. ***(Fabrizio Romano)***

### RODGERS KITITA KIKUBWA
KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers mwenye umri wa miaka 49, atajipatia kitita kinono kama atatimuliwa kutokana na klabu hiyo kuanza vibaya msimu. ***(Mail)***

### ALVAREZ KIPAUMBELE CHELSEA
CHELSEA itanunua kiungo wa kati katika dirisha la Januari huku nyota wa kimataifa wa Mexico, Edson Alvarez mwenye umri wa miaka 24, akiwa ni kipaumbele chao cha kwanza. ***(Standard)***

### MOUNT MKATABA MPYA
CHELSEA wako tayari kumpa mkataba mpya kiungo wao wa England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 23, baada ya mwenzake, Reece James mwenye umri wa miaka 22, kusaini mkataba mpya wa miaka sita. ***(Telegraph)***

### LEAO KUFUNGWA MILAN
KOCHA Mkuu wa AC Milan, Stefan Pioli, amefichua kwamba, klabu hiyo inajiandaa kumpa mkataba mpya mshambuliaji wake, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23, huku kukiwa na ripoti za kuhusishwa na klabu kadhaa ikiwamo Liverpool. ***(Liverpool Echo)***

### KOVACIC NA GVARDIOL
MATEO Kovacic, amesema alimpendekeza beki Mcroatia wa RB Leipzig, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 20 kwenda Chelsea katika dirisha la usajili lililofungwa hivi karibuni. ***(Standard)***

### COSTA ANUKIA WOLVES
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Hispania, Diego Costa mwenye umri wa miaka 33, amesafiri jana kwenda kukamilisha uhamisho wake wa kutua Wolves. ***(Telegraph)***

### CAICEDO ATAJWA BRIGHTON
KLABU ya Brighton inajiandaa kufanya mazungumzo na Liverpool kwa ajili ya uhamisho wa Januari wa kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 20. ***(Tera Deportes, via Express)***

### LAIMER HAKUWA SOKONI
KIUNGO wa RB Leipzig raia wa Austria, Konrad Laimer mwenye umri wa miaka 25, hakuwa na nia ya kusaini dakika za mwisho kwenda Liverpool, licha ya kuzagaa kwa uvumi huo. ***(Standard)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# POGBA HATIHATI KUCHEZA KOMBE LA DUNIA QATAR

Mimi si daktari, ninaamini ninachoambiwa, kutakuwa na wiki hizi tano za...

**PARIS, Ufaransa**

PAUL Pogba ameamua kufanyiwa upasuaji kwenye goti lake huku akikabiliwa na vita ya kuwa fiti haraka kabla ya kuanza kwa Kombe la Dunia.

Kiungo huyo aliumia goti muda mfupi baada ya kurejea Juventus, msimu huu wa majira ya joto, ingawa mwanzoni aliamua kutofanyiwa upasuaji na badala yake akatafuta matibabu mbadala.

Pogba, alirejea mazoezini Jumatatu, lakini imeripotiwa kwamba alifeli mtihani wa utimamu wa mwili na sasa ameamua kufanyiwa upasuaji kitu ambacho kinaweza kumuweka nje kwa takriban miezi miwili.

Ufaransa, itaanza kutetea Kombe la Dunia Novemba 22 dhidi ya Australia, na hivyo kumuacha Pogba akiwa na wakati mchache sana wa kuthibitisha kuwa yuko fiti kabla ya michuano hiyo nchini Qatar.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya uamuzi wa Pogba, Kocha wa Juventus, Massimiliano Allegri, alisema alitarajia Pogba angekosa kucheza kwa takribani wiki tano tu.

"Mimi si daktari, kwa hiyo sijui ni nini bora, ninaamini ninachoambiwa. Kutakuwa na wiki hizi tano za matibabu na kisha tunatumaini atarejea haraka iwezekanavyo," alisema Allegri.

Pogba, alikamilisha kurejea kwake Juve kutoka Manchester United kwa uhamisho wa bure (tena) msimu wa majira ya joto.

Juventus wameonekana kukosa raha katika hali yao ya sasa, wakishinda mechi mbili na kutoka sare tatu kati ya tano za mwanzo.

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,029,4

MECHI KALI

SIMBA
VERSUS
KMC

1 | 1.31
X | 4.62
2 | 8.45

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa · vodacom m-pesa · airtel money · ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HAG: NITAKUWA RAFIKI NA MWALIMU WA RONALDO

**MANCHESTER, England**

KOCHA Erik ten Hag, ameahidi kumpa Cristiano Ronaldo msaada na muda anaohitaji ili kuongeza kasi pamoja na wachezaji wenzake wengine wa Manchester United.

Ronaldo, alikosa mechi nyingi za maandalizi ya msimu mpya na akaomba kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto, lakini amekuwa sehemu ya kikosi katika mechi sita za Ligi Kuu chini ya Ten Hag, akianza mchezo mmoja na akitokea benchi mechi tano.

Huku dirisha la uhamisho likiwa limefungwa na Ronaldo kulazimika kuweka umakini wake pekee kwa United Ten Hag, ameahidi kufanya awezalo kumsaidia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 kurejea katika ubora wake.

"Nitakuwa rafiki yake na wakati mwingine nitakuwa mwalimu wake," alisema Hag, baada ya ushindi wa mabao 3-1dhidi ya Arsenal Jumapili.


"Inategemea na hali ilivyo. Kama tunavyojua wote hakuwa na maandalizi ya msimu mpya na huwezi kukosa maandalizi ya msimu mpya.

"Ni msingi na haswa katika mchezo tunaocheza, njia ya uchezaji. Tunacheza aina nyingine ikilinganishwa na mwaka jana. Inategemea na mahitaji, ushirikiano na nafasi fulani."

Kabla ya mchezo huo, Hag alikiri Ronaldo ni kama mchezaji mwingine kwenye kikosi hicho, atahitaji muda kuzoea aina yake ya uchezaji, akikubali kuwa mshambuliaji huyo yuko nyuma ya kundi kwa sababu ya kufupishwa kwake kwa maandalizi ya msimu mpya.

Pande kadhaa duniani zilihusishwa na Ronaldo, lakini wengi wao walijitokeza hadharani kukana kumtaka mshambuliaji huyo, zikiwamo Bayern Munich, Atletico Madrid na Napoli.

Mkataba wa sasa wa Ronaldo unaendelea hadi mwisho wa msimu, ingawa kuna chaguo kwa United kuongeza muda wa miezi 12.




# Bayern, Liverpool uso kwa uso kwa Gavi

**MUNICH, Ujerumani**

MABINGWA wa Ujerumani Bayern Munich, wamejiunga kwenye kinyang'anyiro cha kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Barcelona, Gavi, kwa mujibu wa Bild.

Gavi ni mmoja wa wachezaji vijana wenye vipaji vya hali ya juu barani Ulaya kwa sasa ambaye amekuwa mchezaji wa kikosi cha kwanza cha Barcelona tangu msimu wa 2021-22.

Kinda huyo tayari ameshaichezea timu ya Taifa ya Hispania mara 10, licha ya kufikisha miaka 18, Agosti mwaka huu.




Hata hivyo, rais wa Barcelona, Joan Laporta, ameripotiwa kupambana kumbakiza mchezaji huyo ili aendelee kuitumikia klabu hiyo, licha ya kwamba hadi sasa bado hawajafikia muafaka kuhusu mkataba mpya.

Mkataba wa Gavi, unamalizika mwishoni mwa msimu huu na tayari anawindwa na Liverpool na Manchester United.

Nao Bayern wamejitoza kuwania saini ya Gavi ambaye viongozi wa 'Blaugrana' wameripotiwa kupambana ili kuhakikisha anabaki.

## HABARI MICHEZO


401,974/-

# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII
## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 10/09/22 | 17:00 | KV Kortrijk vs Yellow-Red KV Mechelen | 2.46 | 3.45 | 2.60 |
| 02. 10/09/22 | 17:00 | Shrewsbury Town vs Oxford United | 2.50 | 3.25 | 2.65 |
| 03. 10/09/22 | 17:00 | Birmingham City vs Swansea City | 2.80 | 3.15 | 2.46 |
| 04. 10/09/22 | 17:00 | Barnsley vs Portsmouth FC | 2.65 | 3.35 | 2.48 |
| 05. 10/09/22 | 17:00 | Southampton FC vs Brentford FC | 2.34 | 3.35 | 2.80 |
| 06. 10/09/22 | 17:00 | Leicester City vs Aston Villa | 2.45 | 3.35 | 2.70 |
| 07. 10/09/22 | 17:15 | Espanyol Barcelona vs Sevilla FC | 2.90 | 3.10 | 2.41 |
| 08. 11/09/22 | 14:30 | KVC Westerlo vs RSC Anderlecht | 2.75 | 3.35 | 2.38 |
| 09. 11/09/22 | 16:00 | West Ham United vs Newcastle United | 2.37 | 3.30 | 2.80 |
| 10. 11/09/22 | 16:00 | Sassuolo Calcio vs Udinese Calcio | 2.60 | 3.40 | 2.48 |
| 11. 11/09/22 | 16:00 | Angers SCO vs Montpellier HSC | 2.45 | 3.40 | 2.65 |
| 12. 11/09/22 | 16:00 | Leixoes SC vs SC Farense | 3.00 | 3.15 | 2.33 |
| 13. 11/09/22 | 16:30 | 1. FC Cologne vs Union Berlin | 2.48 | 3.30 | 2.65 |
| 14. 11/09/22 | 17:15 | Spal Ferrara vs Venezia FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 15. 11/09/22 | 17:30 | FC Pacos Ferreira vs Casa Pia Lisbon | 2.70 | 3.00 | 2.65 |
| 16. 11/09/22 | 21:45 | AS Monaco vs Olympique Lyon | 2.50 | 3.40 | 2.60 |
| 17. 11/09/22 | 22:00 | Real Betis Seville vs Villarreal CF | 2.60 | 3.25 | 2.55 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 07/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1925 | Jeonbuk Hyundai vs FC Seoul | 2.15 | 3.33 | 2.99 |
| 13:00 | 2667 | Vissel Kobe vs Kashima Antlers | 2.66 | 3.15 | 2.45 |
| 13:00 | 3649 | Kyoto Sanga vs Tokyo Verdy | 2.22 | 3.15 | 3.00 |
| 13:00 | 5102 | Yokohama F Marinos vs Shonan Bellmare | 1.61 | 3.93 | 4.43 |
| 13:00 | 5771 | Avispa Fukuoka vs Ventforet Kofu | 1.81 | 3.28 | 4.11 |
| 13:30 | 1001 | Daegu vs Seongnam Ilhwa | 1.96 | 3.44 | 3.34 |
| 13:30 | 2218 | Ulsan Hyundai vs Suwon Samsung | 1.50 | 4.01 | 5.48 |
| 16:00 | 3478 | Mtibwa Sugar vs Ihefu FC | 1.76 | 3.05 | 4.91 |
| 16:00 | 4178 | Velez Sarsfield Reserve vs Arsenal FC Reserve | 1.51 | 3.94 | 5.51 |
| 16:00 | 5385 | Kiyovu Sports vs Espoir FC | 1.29 | 4.52 | 9.83 |
| 17:00 | 1878 | Gimnasia de la Plata Reserve vs Newells Old Boys | 2.07 | 3.19 | 3.29 |
| 17:00 | 3759 | Pumas U20 vs Queretaro U20 | 1.43 | 4.42 | 5.69 |
| 17:00 | 4090 | FK Tikves Kavadarci vs Shkupi Skopje | 4.02 | 2.94 | 1.95 |
| 17:00 | 4572 | Puebla U20 vs Pachuca U20 | 2.85 | 3.63 | 2.11 |
| 17:00 | 5391 | Mes Shahr-e Babak vs Shahrdari Hamedan | 2.20 | 2.75 | 3.80 |
| 17:15 | 4709 | Saipa Karadj vs Kheybar Khorramabad FC | 2.63 | 2.68 | 2.88 |
| 17:30 | 1398 | Shams Azar Qazvin vs Pars Jonoubi Jam | 2.40 | 2.66 | 3.25 |
| 17:30 | 5221 | Sloboda Tuzla vs Zrinjski Mostar | 6.49 | 3.74 | 1.47 |
| 18:00 | 1425 | Be1 NFa vs FA Siauliai B | 1.43 | 4.44 | 5.72 |
| 18:00 | 2870 | Zalgiris Kaunas vs Dziugas | 1.32 | 4.70 | 7.64 |
| 18:00 | 3713 | Mazatlan FC U20 vs Atlas U20 | 1.75 | 4.10 | 3.52 |
| 18:40 | 4010 | Alshoulla vs Jeddah Club | 1.93 | 2.99 | 4.02 |
| 19:00 | 1632 | Simba vs KMC | 1.31 | 4.62 | 8.45 |
| 19:00 | 5096 | Lietava Jonava vs Banga Gargzdai | 6.87 | 4.42 | 1.37 |
| 19:30 | 3586 | St.Pauli II vs FC Teutonia 05 | 3.93 | 3.69 | 1.74 |
| 19:30 | 4624 | CSD Barnechea vs Cobreloa | 2.76 | 3.01 | 2.47 |
| 19:30 | 4964 | Nykobing FC vs Odense | 5.91 | 4.33 | 1.43 |
| 19:45 | 4496 | Ajax vs Rangers | 1.45 | 4.62 | 5.82 |
| 19:45 | 5749 | Eintracht Frankfurt vs Sporting Lisbon | 2.09 | 3.51 | 3.15 |
| 20:00 | 1562 | Lorient vs Lyon | 4.33 | 4.13 | 1.66 |
| 20:00 | 2329 | SV Neuhof vs SV Steinbach 1920 | 1.85 | 4.22 | 3.09 |
| 20:00 | 3121 | TUS Dietkirchen vs 1. Hanauer FC 93 | 3.24 | 4.32 | 1.79 |
| 20:00 | 3589 | SC 1929 Waldgirmes-Rot vs Weiss Hadamar | 2.04 | 3.55 | 3.05 |
| 20:00 | 4678 | FC Ashdod vs Beitar Jerusalem | 2.95 | 2.76 | 2.51 |
| 20:00 | 5185 | FK Panevezys vs Vilniaus Riteriai | 2.16 | 3.18 | 3.09 |
| 20:00 | 5682 | Eintracht Stadtallendorf vs TSV Steinbach II | 1.13 | 7.80 | 14.00 |
| 20:20 | 2774 | Al Ahli Doha SC vs AL Wakrah | 4.71 | 3.93 | 1.58 |
| 20:30 | 1649 | Hamrun Spartans vs Marsaxlokk FC | 1.37 | 4.61 | 6.47 |
| 20:30 | 5148 | Chippa Utd vs Mamelodi Sundowns | 5.21 | 3.41 | 1.68 |
| 22:00 | 1703 | Brugge vs Bayer Leverkusen | 3.00 | 3.74 | 2.09 |
| 22:00 | 2252 | Atletico Madrid vs Porto | 1.79 | 3.40 | 4.40 |
| 22:00 | 3557 | Always Ready vs Guabira Montero | 1.17 | 6.50 | 10.83 |
| 22:00 | 4053 | Barcelona vs Viktoria Plzen | 1.08 | 8.86 | 23.35 |
| 22:00 | 4605 | Napoli vs Liverpool | 3.45 | 3.60 | 1.95 |
| 22:00 | 4657 | Tottenham vs Marseille | 1.46 | 4.30 | 6.19 |
| 22:00 | 5898 | Inter vs Bayern Munchen | 3.65 | 3.95 | 1.81 |
| 22:15 | 3754 | Vikingur Reykjavik vs Leiknir | 1.23 | 5.87 | 8.42 |
| 22:30 | 5656 | Univ de Chile vs Coquimbo | 2.10 | 3.23 | 3.19 |
| 23:00 | 3132 | Atletico Mineiro vs Bragantino SP | 1.59 | 3.63 | 5.10 |
| 23:00 | 3962 | FC Aguablanca vs Leones FC | 2.35 | 2.72 | 3.25 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KOCHA MFARANSA WA AZAM KUANZIA ALIPOACHIA MOALLIN

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC imesema kocha wao mpya, Denis Lavagne, iliyetangazwa juzi usiku na kuwasili nchini jana asubuhi, atafanya kazi na makocha atakayewakuta kwa sababu wanataka kuendeleza walichonacho na si kuanza upya.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka Zakazi', alisema kocha huyo raia wa Ufaransa amekuja peke yake na wasaidizi wataendelea kuwa wale wale ambao walikiongoza kikosi baada ya kuondolewa kwa kocha Abdihamid Moallin.

"Anakuja yeye kwanza, anafanya kazi na anaowakuta, hayo mengine tutazungumza huko mbele, hatutaki kuanza tena upya, tunachotaka ni kuendeleza kile tulichonacho," alisema Zaka Zakazi.

Kuhusu sifa za kocha huyo, Zakazi alisema ni kocha mkubwa mwenye mafanikio ndani ya nchi alizozifundisha pamoja na nje, mwenye kulifahamu soka la Kiafrika.

"Ni kocha mkubwa sana, kocha ambaye amefanikiwa ndani ya nchi alizokuwa anazifundisha na nje ana rekodi nzuri, lakini analijua soka la Afrika, amekuja tangu 2007 na hajaondoka Afrika, amefundisha kwenye kanda zote za Afrika, na hiyo siyo faida kwake tu, bali hata kwetu Azam FC." alisema.

Mfaransa huyo amewahi kufundisha timu ya Taifa ya Cameroon 2011 hadi 2012, USM Alger na JS Kabylie zote za Algeria, Etoile Du Sahel (2013), Smouha ya Misri, Coton Sports (Cameroon) na Al Hilal ya Sudan.

Moja ya mafanikio yake makubwa ni kufika fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2008 akiwa na Coton Sport ya Cameroon na kupoteza dhidi ya Al Ahly ya Misri kwa jumla ya mabao 4-2.




Kocha Mkuu mpya wa Azam FC, Denis Lavagne

# SMZ yashauriwa kunusuru Sauti za Busara

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imeshauriwa kuangalia njia ya kuliokoa Tamasha la Kimataifa la Sauti za Busara Zanzibar kuwa katika hatari ya kutokufanyika baada ya mradi wa ujenzi wa hoteli ya nyota tano, Blue Amber kusitisha mkataba wa udhamini uliofikiwa Machi mwaka huu.

Taarifa zinaeleza kuwa kampuni hiyo imechukua hatua hiyo siku chache baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kusitisha ujenzi wa mradi wa Blue Amber, uliokuwa unafanyika Matemwe Mbuyutende Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Akizungumza na Waandishi wa Habari Ofisini kwake Maisara, Mkurugenzi Mtendaji wa tamasha hilo, Yussuf Mahmoud, alisema wamepokea kwa mshituko mkubwa hatua ya wafadhili kujiondoa na kwamba kutasababisha kuumia kiuchumi. "Tulikuwa tufanye tamasha la 20 tangu kuanzishwa mwaka 2003, lakini tumepokea kwa mshtuko mkubwa baada ya wafadhili wetu mradi wa Ujenzi Blue Amber kujiondoa katika udhamini ghafla," alisema Yussuf.

Wafadhili walikuwa na mkataba wa udhamini wa miaka mitatu mpaka mwaka 2025 kabla ya kupata ufadhili huo walikuwa wakidhaminiwa na Ubalozi wa Norway kuanzia mwaka 2009 kabla ya kumaliza muda wao Machi mwaka huu.

"Tamasha la Sauti za Busara ni kitu kikubwa kwa Zanzibar na Afrika katika kutangaza sekta ya utalii na kuwaunganisha wasanii kutoka mataifa mbalimbali duniani na kutoa ajira kwa vijana na wajasiliamali Zanzibar.

Alisema, Dola 500,000 za Marekani zinahitajika ili tamasha liweze kufanyika Febuari mwakani, lakini mpaka sasa hakuna wafadhili waliojitokeza hivyo kuendelea kubakia njiapanda.

Yussuf, alisema utafiti unaonyesha Tamashara la Busara linapofanyika huchangia karibu Dola milioni 18 za Marekani kupitia sekta ya utalii na huduma za usafiri kwa watalii na wanaotembelea visiwani Zanzibar.

# Michezo

Jumatano Septemba 7, 2022

Nipashe






**Pogba hatihati kucheza Kombe la Dunia Qatar**

KWAHERINI...



Aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Zoran Maki.

# Zoran atoa neno kuondoka Simba

## ●●●Atangazwa rasmi Al Ittihad ya Misri, uongozi Msimbazi wafunguka mazito ya mrithi wake...

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba leo ikishuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha KMC FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara huku zikiwa zimebaki siku nne kuanzia leo kabla ya kuvaana ugenini na Nyasa Big Bullets ya Malawi kwenye mchezo wa awali wa Ligi ya Mabingwa Afrika, imeachana na Kocha wake Mkuu, Zoran Manojlovic 'Maki', na bila kuchelewa akatoa neno la upendo kwa Wanamsimbazi hao.

Simba ambayo itaanzia ugenini kwenye mechi hiyo ya awali Jumamosi wiki hii, imepata pigo kubwa baada ya kuachana na Zoran pamoja na wasaidizi wake, Kocha wa Viungo, Sbai Karim na Kocha wa Makipa, Mohammed Rachid, hivyo timu kwa sasa kubaki chini ya Kocha Msaidizi, Seleman Matola.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wamefikia makubaliano ya pande zote mbili ya kuvunja mkataba na kocha huyo pamoja na wasaidizi wake hao wawili, Sbai na Rachid.

"Uongozi wa Simba unawashukuru makocha hao kwa mchango wao ndani ya klabu yetu na inawatakia kila la kheri katika majukumu yao mapya, tayari mchakato wa haraka wa kutafuta makocha wapya umeanza na utakamilika hivi karibuni.

"Muda ni mfupi, lakini tunajitahidi kwa kasi inayowezekana ili tuweze kupata kocha kwa haraka, hadi kufika tarehe 10 (mwezi huu), kutakuwa na mabadiliko kwenye benchi la ufundi, kuna timu ipo kazini kutafuta warithi wao. Hili limekwisha Wanasimba, tukutane kwa Mkapa," alisema Ahmed.

"Kwa bahati nzuri msimu uliopita alipoondoka Didier Gomes, mechi ya kwanza kucheza bila kocha mkuu na kuwa chini ya Matola ilikuwa na KMC na kila mtu anajua kilichotokea, tuliwafunga mabao 3-1, safari hii imetokea tena, Zoran anaondoka mechi ya kwanza tunacheza tena na hao hao KMC chini ya Matola."

Alisema kulingana na ubora wa wachezaji waliosajiliwa ndani ya klabu hiyo, kocha yeyote atakayekuja anaweza kufundisha Simba na kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yao.

Wakati Simba ikieleza hayo, Zoran kupitia ukurasa wake wa Instagram hakuwa na maneno mengi zaidi ya kuandika: "Ukweli napenda kuishukuru klabu hii kwa kunipa nafasi ya kipekee. Asante kwa wote walioniamini na ninashukuru kwa kila kitu".

Hata hivyo, jana hiyo hiyo, Klabu ya Al Ittihad Alexandria ya Misri ilitangaza kuingia mkataba wa mwaka mmoja na Zoran, ambaye inaelezwa aliondoka nchini jana.

Katika hatua nyingine, kuelekea mchezo wa leo, Matola amesema Simba itamkosa beki wake wa kimataifa, Joash Onyango ambaye hakuwapo katika programu ya mazoezi kwa siku mbili za maandalizi ya mchezo huo.

"KMC FC ni timu nzuri pia ni wagumu, lakini hata wakiwa wagumu kiasi gani tunalazimika kupambana hadi tone la mwisho kesho (leo)kupata pointi tatu muhimu dhidi ya wapinzani wetu hao," alisema Matola.

Naye Kocha Msaidizi wa KMC FC, Ahmad Ally, alisema maandalizi kwa ujumla wako fiti kwa asilimia 90 na zilizobaki ni uwanjani tu.

"Simba ni timu nzuri na bora ina wachezaji wazuri na muda wowote wanaweza kukupa matokeo, hilo tumefanyia kazi na tutacheza kwa nidhamu kubwa."

## Yanga yakoleza moto kwa Kisinda

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga bado inaonekana kumpigania mchezaji wake mpya iliyomsajili kutoka RS Berkane, Tuisila Kisinda kuingia kwenye mfumo wa usajili badala ya Lazarous Kambole, ambaye ilimsajili kutoka Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Yanga imeeleza kupeleka maombi kufanyika mabadiliko hayo mbele ya Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji, licha ya Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuzuia usajili huo.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Simon Patrick, amesema wamepeleka maombi yao mbele ya Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji kwa sababu ndiyo wenye mamlaka ya kutoa au kuzuia leseni na si mtu mwingine yeyote.

**"Si kweli kwamba tumezidisha idadi ya wachezaji ila tuliomba tumwondoe mchezaji mmoja, baada ya madaktari kuthibitisha kuwa Kambole ana majeraha na tunataka kuingiza jina la Kisinda, tumeomba ndani ya muda, dirisha la usajili lilikuwa halijafungwa na TFF hiyo ikatusaidia kupata Hati ya Uhamisho ya Kimataifa (ITC) na tukaipata kabla ya dirisha la usajili kufungwa.**

"Kilichobaki tumepeleka maombi yetu mbele ya Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji kwa sababu ndiyo yenye mamlaka na kutoa na kuzua leseni, basi tunaiachia yenyewe ifanye maamuzi, na sisi tumeomba waitoe leseni ya Kambole na kuikubali ya Kisinda.

"Tunaiomba Kamati kwa sababu ina mamlaka hiyo chini ya kifungu cha 67 kifungu kidogo cha 13, kama ikiamua kukataa basi. Kamati ni huru ina watu wenye weledi na najua watalifanyia kazi," alisema Ofisa Mtendaji huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >